JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**WIZARA YA AFYA NA USTAWI WA JAMII**

# SERA YA AFYA

**Juni, 2007**

# YALIYOMO


**TAFSIRI……………………………………………………………………………. vii**

**DIBAJI…………………………………………………………………………..…. ix**

**1.0 UTANGULIZI………………………………………………..…..…… 1**

**2.0 HALI YA HUDUMA ZA AFYA NCHINI……………………………….…. 2**

2.1 HUDUMA ZA AFYA KABLA NA BAADA YA UHURU……..…… 2

2.2 UTEKELEZAJI WA SERA YA MWAKA 1990……………………. 3

2.2.1 Mafanikio…………………………………………………… 3

2.2.2 Upungufu…………………………………………………… 4

2.2.3 Changamoto………………………………………………… 5

**3.0 UMUHIMU WA SERA…………………………………………..…..…. 7**

**4.0 DIRA, MAKUSUDIO NA MADHUMUNI YA SERA…………………… 8**

4.1 DIRA……………………………………………….………...… 8

4.2 MAKUSUDIO……………………………………………..… 8

4.3 MADHUMUNI……………………………………………...…. 8

4.3.1 Madhumuni mahsusi………………………………….……… 8

**5.0 HOJA ZA SERA NA MATAMKO……………………………….……… 10**

5.1 AFYA YA MSINGI……………………………………………..… 10

5.2 UBORESHAJI NA UDUMISHAJI WA AFYA…………………… 11

5.2.1 Elimu ya afya………………………………………………… 11

5.2.2 Uhamasishaji na Ushirikishaji…………………………..…… 12

5.2.3 Afya ya Mazingira……………………………..………. 13

5.2.4 Afya kazini…………………………………………………… 14

5.2.5 Lishe……………………………………………….……..…… 14

5.3 KINGA…………………………………………………………………. 15

5.3.1 Udhibiti wa magonjwa………………………………….…..…… 15

5.3.2 Magonjwa ya Kuambukiza na milipuko……………………… 16

5.3.3 Magonjwa yasiyo ya kuambukiza na ajali…………………… 17

5.3.4 Afya ya Mama na Mtoto…………………………………….…. 18

5.3.5 Afya ya Uzazi……………………………………………….…. 20

5.4 TIBA…………………………………………………………………… 20

5.4.1 Mfumo wa utoaji huduma za afya kwa uwiano wa kijiografi ... 22

5.4.2 Uuguzi na Ukunga……………………………….….….…… 23
5.4.3 Dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi……………………..… 24
5.4.4 Uchunguzi wa magonjwa kwa njia ya maabara na radiolojia 25
5.4.5 Afya ya Kinywa……………………………………………..… 25
5.4.6 Damu salama………………………………………………… 26
5.4.7 Dawa za Kulevya na Afya ya Akili…………………………… 27
5.4.8 Ushirikishaji ,Uchangiaji na Msamaha wa Huduma za Afya. 28
5.4.9 Ushirikishaji wa mashirika ya dini, asasi zisizo za kiserikali
na sekta binafsi…………………………………….…….…. 30
5.4.10 Huduma za afya binafsi………………………………………. 31
5.4.11 Tiba Asilia, Tiba Mbadala na Ukunga wa Jadi…….………. 32
5.5 HUDUMA ZA UTENGEMAO……………………………….………… 32
5.6 MAENDELEO YA WATUMISHI NA VYUO VYA MAFUNZO
VYA SEKTA YA AFYA…………………………………..…….. 33
5.6.1 Maendeleo ya watumishi…………………………..…… 33
5.6.2 Vyuo vya mafunzo ya afya………………………………..… 34
5.7 RASLIMALI………………………………………………………… 35
5.7.1 Watu……………………………………………………...…… 35
5.7.2 Fedha………………………………………………………… 36
5.8 MIPANGO YA AFYA……………………………………………… 37
5.8.1 Mipango na Uratibu…………………………………..……… 37
5.8.2 Ubora na viwango vya huduma………………………………. 38
5.8.3 Ufuatiliaji na tathmini……………………………………...… 39
5.8.4 Ukusanyaji na utumiaji wa takwimu………………………… 39
5.8.5 Utafiti………………………………………………………… 40
5.9 HUDUMA NYINGINE……………………………………………… 41
5.9.1 Udhibiti wa kemikali na uchambuzi wa chembe hai na
Viinitata……………………………………………………. 41
5.9.2 Usimamizi na udhibiti wa ubora wa chakula, dawa,
vipodozi, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi…………………. 42
5.9.3 Udhibiti wa kemikali, uchchunguzi wa sampuli
mbalimbali na matumizi ya vinasaba……………………..….. 43

5.10 WAKALA NA TAASISI ZILIZOPO CHINI YA WIZARA……..… 44
5.10.1 Bohari ya Dawa ya Serikali……………………………..… 44
5.10.2 Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu…………..… 44
5.10.3 Wakala wa Maabara ya Mkemia wa Serikali……………… 45
5.10.4 Mamlaka ya Chakula na Dawa…………………………… 46
5.10.5 Taasisi ya Chakula na Lishe……………………………….. 46
5.10.6 Taasisi ya Saratani ya Ocean Road………………………… 47
5.10.7 Taasisi ya Mifupa MOI……………………………………..… 48
5.10.8 Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya………………………… 49
5.10.9 Hospitali ya Taifa ya Muhimbili…………………………… 50
5.11 MABARAZA NA VYAMA VYA KITAALUMA……………………. 51
5.11.1 Mabaraza ya kitaaluma…………………………………..… 51
5.11.2 Vyama vya kitaaluma……………………………………… 51
**6.0 MASUALA MTAMBUKA YA SERA…………………………..……. 53**
6.1 MAJANGA NA MAAFA…………………………………………… 53
6.2 USHIRIKIANO WA KIKANDA NA KIMATAIFA……………..… 54
6.3 UKIMWI……………………………………………………..…… 54
6.4 TEKNOLOJIA YA HABARI NA MAWASILIANO (TEKNOHAMA)……………………………………………………. 55
6.5 UTAWALA BORA…………………………………………..…… 56
6.6 JINSIA……………………………………………………..……. 57
6.7 KUPUNGUZA UMASKINI…………………………………….… 58
6.8 HAKI ZA BINADAMU……………………………………..… 58
6.9 RUSHWA…………………………………………………….… 59
6.10 MAZINGIRA……………………………………….……….. 59
**7.0 MUUNDO WA KITAASISI**……………………………………..… 61
7.1 MUUNDO NA MAJUKUMU YA UTOAJI HUDUMA KATIKA KILA NGAZI ………………………………………………..…… 61
7.1.1 Kaya, Mtaa/Kijiji……………………………………..…..…… 61
7.1.2 Kata…………………………………………………...……. 62
7.1.3 Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa na za Jiji……...…… 62
7.1.4 Mkoa……………………………………………………. 63
7.1.5 Kanda………………………………………………………. 64

7.1.6 Taifa……………………………………………………....…. 64

7.2 USHIRIKIANO NA WADAU MBALIMBALI……………….…..…. 65

7.2.1 Mashirika ya dini…………………………………………….. 65

7.2.2 Sekta binafsi………………………………………………….. 65

7.2.3 Asasi zisizo za kiserikali……………………………………… 66

7.2.4 Mashirika ya kimataifa na nchi wahisani…………………….. 66

**8.0 MFUMO WA KISHERIA……………………………………...…… 67**

8.1 SHERIA ZA KUSIMAMIA HUDUMA ZA AFYA…………….…. 67

8.2 VYOMBO VYA KISHERIA VYA KUSIMAMIA HUDUMA ZA AFYA……………………………………………………………….. 67

8.3 SHERIA YA KUSIMAMIA VYUO VYA MAFUNZO YA AFYA…………………………………………..…………...…. 68

9.0 MWISHO…………………………………………………...…. 69

# TAFSIRI

| Neno | Tafsiri |
|---|---|
| Afya | Ukamilifu wa binadamu kimwili, kiakili na kijamii na kutokuwepo kwa maradhi |
| Bioanuai | Aina mbalimbali za maisha ya viumbe hai, jinsi vinavyoishi katika mifumo ya maisha. |
| Chembe hai na viini tete | Chembe hai ni seli na Viini tete ni viini vilivyobadilishwa kijenetiki, vinavyoweza kuhifadhiwa na kurutubishwa kwa ajili ya kupata kiumbe kipya pasipo kukutana kwa mbegu ya kiume na yai la kike. Vile vile, viini tete hivyo vyaweza kutumika kutibu magonjwa kama kansa na ukuaji usio kawaida wa chembe hai (*abnormal growth*). |
| Huduma za utengemao | Humaanisha huduma zinazomwezesha mtu mwenye matatizo ya kijamii, kumudu maisha yake ya kila siku na pia kushiriki kikamilifu katika kuiletea maendeleo jamii inayomzunguka. |
| Ithibati | Ni hati ya kutambulika baada ya kufikia viwango vilivyowekwa. |
| Masuala mtambuka | Ni yale ambayo utekelezaji wake unagusa sekta mbalimbali na jamii. |
| Matamko | Ni azma ya Serikali inayoelekeza kufikia malengo iliyojiwekea. |
| Sera | Ni tamko lenye kusudio la kufikia lengo au madhumuni maalum. |
| Taaluma mseto | Kuwa na wataalam wenye taaluma mbalimbali katika kituo cha kutolea huduma za afya. |
| TEKNOHAMA | Ni kifupisho cha 'Teknolojia ya Habari na Mawasiliano.' |
| Tofauti kati ya upungufu na changamoto | Upungufu ni tatizo lililopo na changamoto ni namna ya kukabiliana na tatizo. |

| **Neno** | **Tafsiri** |
|---|---|
| Tofauti ya ‘tiba asili’ na ‘tiba mbadala’. | Tiba ya asili ni matibabu ya kijadi yanayorithishwa toka kizazi kimoja hadi kingine kwa njia ya mdomo au maandishi, tiba mbadala ni tiba isiyotumia upasuaji au dawa kwa mfano mazoezi ya viungo, kuchoma kwa mionzi na kuchoma visindano. |
| Uwiano | Upatikanaji wa huduma za afya kulingana na mahitaji halisi |
| Vinasaba (DNA – Deoxyribonucleic acid) | Ni chembechembe za asili za urithi pia, chembechembe zinazotumika kutambua chanzo cha tukio, magonjwa ya urithi na kutambua mzazi halali wa mtoto. |
| Vitendanishi | Ni kemikali zinazotumika katika uchunguzi wa kimaabara. |

# DIBAJI

Serikali imeendelea kutoa kipaumbele katika huduma za afya zenye ubora na zinazowafikia wananchi wote ili kuboresha afya zao. Serikali inatambua umuhimu wa afya bora kwa wananchi wake kwani afya bora ni raslimali muhimu kwa maendeleo. Maendeleo ya Taifa letu la Tanzania yataletwa na wananchi wenye afya na wenye uwezo wa kuzalisha mali.

Katika kuhakikisha kuwa wananchi wana afya bora, Serikali imeendelea kushirikiana na wadau mbalimbali kutoa huduma za afya kwa kuzingatia sera na miongozo iliyopo.

Sera ambayo imeendelea kutumika katika kuelekeza utoaji wa huduma za afya ilipitishwa mwaka 1990. Tangu sera hiyo ilipopitishwa, yamekuwepo mabadiliko mbalimbali ya kiuchumi na kijamii, mabadiliko ya sayansi na technolojia na kuongezeka kwa magonjwa. Yametokea pia, maelekezo mbalimbali ya Serikali. Mabadiliko na maelekezo yote haya yanatoa changamoto mpya katika utoaji wa huduma za afya na yamechangia kwa pamoja kuifanya sera iliyopitishwa mwaka 1990 kutokidhi mahitaji na matarajio ya sasa na ya miaka ijayo.

Mfumo na utaratibu wa utoaji huduma unaotumika hivi sasa umebadilika kutokana na mabadiliko yaliyotokea, ikilinganishwa na mfumo uliokuwa unatumika kwa maelekezo ya Sera ya 1990. Mwaka 1996 marekebisho ya sera yalipitishwa kwa lengo la kuanzisha mfumo mpya wa utoaji na uendeshaji wa huduma za afya katika ngazi ya wilaya. Katika marekebisho haya, ushiriki wa sekta binafsi katika utoaji wa afya ulitambuliwa na kupewa msukumo, pia yalikasimu usimamizi wa utekelezaji katika mamlaka za Serikali za Mitaa na hivyo kuongeza ushiriki wa wananchi katika kusimamia na kumiliki raslimali za afya.

Mabadiliko haya yamelazimu kufanyia mapitio ya Sera ya mwaka 1990, na yamezingatia sera na mikakati mbalimbali ya kitaifa na kimataifa. Sera na mikakati hiyo ni pamoja na Dira ya Maendeleo ya Taifa ya 2025, Malengo ya Maendeleo ya Milenia na Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA).

Sera ya afya ya mwaka 1990 iliyopitiwa mwaka 2007, imeweka bayana dira, makusudio, maelekezo ya Serikali katika mfumo wa matamko, mabadiliko ya kiuchumi na kijamii, matokeo ya tafiti na majaribio na uzoefu katika utoaji wa huduma. Aidha, utayarishaji wa sera hii umekuwa shirikishi kwa Wizara kuwashirikisha wadau mbalimbali wanaotoa na kutumia huduma za afya katika kupitia Sera ya 1990.

Jukumu la wadau wote wa sekta ya afya ni kusoma, kuielewa na kutafsiri matamko yaliyomo katika sera hii wakati wa kupanga, kutoa na kutathmini huduma za afya nchini.

Wizara inatoa shukrani kwa wadau wote walioshiriki kutoa maoni yao na hivyo kukamilisha Sera hii. Nina imani kuwa wadau katika ngazi zote watashiriki kikamilifu katika kutekeleza Sera hii kwa lengo la kuboresha huduma za afya kote nchini.

Prof. David Homeli Mwakyusa (Mb),
**Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii**

# SERA YA AFYA

## 1.0 UTANGULIZI

Afya maana yake ni hali ya ukamilifu kimwili, kiakili, kijamii na kutokuwepo kwa maradhi. Afya bora ni nguzo na raslimali muhimu katika kuchangia maendeleo ya mtu binafsi, familia na nchi hususan katika kuleta maisha bora na kupunguza umaskini. Kwa mantiki hii afya inalenga kuwa na ustawi endelevu kwa jamii, kwa kuzingatia mchango wa mtu binafsi kulingana na nafasi, uwezo na fursa zilizopo katika kuleta maisha bora. Upatikanaji wa afya bora unahitaji uwezeshaji wa jamii iwe na uwezo wa kushiriki, kuamua, kupanga na kutekeleza mikakati yao ya kuwaletea maendeleo katika ngazi mbalimbali.

Mara baada ya Uhuru (1961) hadi mwaka 1990, Wizara ya Afya imetekeleza huduma za afya nchini kwa kutumia sera ya nchi kwa ujumla bila kuwepo sera rasmi ya Taifa ya Afya. Sera ya nchi ilikuwa ni kupambana na maradhi, ujinga na umaskini. Kwa hiyo mipango yote ya sekta ya afya ililenga katika kupunguza maradhi na vifo kwa kutumia raslimali zilizopatikana.

Sera rasmi ya Afya ilitayarishwa na kupitishwa mwaka 1990. Msisitizo wa sera hii ulikuwa ni kuinua hali ya afya kwa wananchi wote na kipaumbele kilitolewa kwa makundi yaliyo katika hatari zaidi ya kuugua, ambayo ni; watoto wenye umri chini ya miaka mitano, wanawake wajawazito na wananchi wote. Aidha, sera ililenga kuweka mfumo wa huduma za afya utakaokidhi mahitaji ya wananchi na kuongeza umri wa kuishi wa watanzania.

Sera ya Afya ya mwaka 1990 ina upungufu kutokana na mabadiliko ya kiuchumi na kijamii yanayoendelea, maelekezo mapya ya Serikali, kuongezeka kwa magonjwa yakijumuisha mapya na sugu yanayohitaji tiba ya muda mrefu, magonjwa yanayojitokeza uzeeni na mabadiliko katika sayansi na teknolojia. Hivyo, imelazimu kufanya mapitio, ili kuwa na sera inayokidhi mahitaji ya sasa na baadaye.

Sera hii ya Afya ya mwaka 2007, imetayarishwa kwa kuzingatia mabadiliko ya Sera za kiuchumi na kijamii yaliyojitokeza kitaifa na kimataifa. Misingi ya sera hii ni pamoja na Sera ya Afya ya mwaka 1990, Mabadiliko katika Sekta ya Afya, Dira ya Maendeleo ya Taifa ya 2025, Malengo ya Maendeleo ya Milenia na Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania.

## 2.0 HALI YA HUDUMA ZA AFYA NCHINI

Huduma za afya nchini zimeendelea kutolewa kwa kiwango cha kuridhisha kutokana na mabadiliko endelevu yanayofanyika katika Sekta ya afya kwa lengo la kuleta uwiano katika upatikanaji wa huduma bora za afya mijini na vijijini. Kiasi cha asilimia themanini ya watanzania kufikia miaka ya tisini, tayari wana fursa ya kupatiwa huduma katika umbali wa kilomita kumi. Hata hivyo, hali ya afya ya wananchi wengi imeendelea kuwa ya wastani kutokana na changamoto zinazoendelea kujitokeza kabla na baada ya uhuru katika mfumo wa huduma za afya. Hali hii imesababisha kupungua kwa kasi ya kufikia malengo yaliyotarajiwa na serikali.

### 2.1 Huduma za Afya Kabla na Baada ya Uhuru

Kabla ya Uhuru, huduma za afya nchini zilikuwa zinatolewa zaidi kwenye maeneo ya shughuli za kiuchumi kama miji na mashamba makubwa. Baada ya uhuru, Serikali iliweka msukumo zaidi katika kupanua huduma za afya ili kuwafikia wananchi wengi hasa walioko vijijini. Ili kufanikisha azma hii, Serikali iliweka mfumo wa rufaa wa huduma za afya. Kwa mfumo huu, zahanati, vituo vya afya, hospitali za wilaya, hospitali za mikoa, maalum, kanda na taifa zilianzishwa.

Aidha, Serikali ilihamasisha na kuwezesha hospitali za mashirika ya kidini kushirikiana nayo kutoa huduma kwa wananchi. Kipaumbele kilikuwa katika utoaji wa huduma za tiba zaidi kuliko kinga.

Katika kipindi chote hicho hadi miaka ya tisini, huduma za afya zilitolewa bila malipo. Kutokana na hali mbaya ya kiuchumi, Serikali ilianzisha mabadiliko katika Sekta ya Afya ikiwa ni pamoja na ushirikishwaji wa wananchi katika kuchangia gharama za huduma za afya mwaka 1993. Hata hivyo, makundi maalum ambayo ni; wazee wasiojiweza, watu wenye ulemavu, watoto wenye umri chini ya miaka mitano na wanawake wajawazito hawachangii. Serikali imeendelea kuimarisha huduma za afya kwa kushirikisha sekta binafsi.

Hali ya afya ya wananchi wa Tanzania imeendelea kuboreshwa baada ya Uhuru. Hata hivyo kuna baadhi ya makundi ya wananchi ambayo yanahitaji kupewa kipaumbele ili kuendelea kuboresha afya zao kwa kuimarisha mfumo wa utoaji huduma. Wastani wa maisha ya Mtanzania ni miaka 51, yaani miaka 50 kwa wanaume na 52 kwa wanawake. Juhudi zilizopo zitaendelea kuboresha wastani huo.

Watanzania wanakabiliwa na magonjwa makubwa ya kuambukiza ambayo ni UKIMWI, malaria na kifua kikuu. Aidha, afya ya uzazi na mtoto bado hairidhishi. Vile vile, magonjwa yasiyo ya kuambukiza yameanza kujitokeza kwa wingi kutokana na mabadiliko ya mienendo na tabia ya kuishi. Magonjwa haya ni kama saratani, shinikizo la damu, kiharusi na kisukari.

## 2.2 Utekelezaji wa Sera ya mwaka 1990

Sera ya mwaka tisini ilitoa kipaumbele katika utoaji huduma za kinga, tiba, uhamasishaji na utengemao. Huduma hizi zilitolewa kwa kushirikiana na wadau mbalimbali. Katika kutoa huduma za kinga, Serikali imeelekeza mapambano yake katika kutokomeza magonjwa yanayosababisha vifo vya watoto wenye umri chini ya mwaka mmoja na miaka mitano na wanawake wajawazito. Katika utoaji wa huduma hizo, msisitizo umeelekezwa katika utoaji wa chanjo, elimu ya afya na kuruhusu upatikanaji huduma hizo bila malipo. Aidha, Serikali inaendelea na jitihada za kudhibiti na kuzuia magonjwa ya kuambukiza na yasiyo ya kuambukiza.

Huduma za tiba zimeendelea kutolewa katika ngazi zote. Serikali imeendelea kuhakikisha kuwa; dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi vinapatikana na kusambazwa katika vituo vyote vya kutolea huduma. Serikali pia, kwa kushirikiana na wadau imeendelea kuboresha miundombinu ya kutolea huduma za afya katika ngazi zote. Katika kuboresha huduma, mafunzo mbalimbali yamekuwa yakitolewa kwa watumishi kufuatana na taaluma zao na mahitaji. Vilevile, Serikali imeendelea kutoa huduma kwa makundi maalum. Aidha, jamii imeendelea kushirikishwa kikamilifu katika kutambua, kupanga na kutekeleza mipango ya afya ikiwemo usafi wa mazingira na usafi wa mtu binafsi.

Serikali imeendelea kupambana na janga la UKIMWI na magonjwa mengine ya kuambukiza na yasiyo ya kuambukiza, kwa kuanzisha na kutekeleza mikakati maalum ya kuelimisha jamii ili kupunguza maambukizi mapya, kujikinga na kuchukua hatua ya matibabu sahihi mapema. Serikali pia, imekuwa inaendeleza huduma za utengemao kwa kutoa vifaa vya kujimudu, elimu ya kuwawezesha watu wenye ulemavu kujitegemea na kutoa huduma za tiba na kinga.

### 2.2.1 Mafanikio

Utekelezaji wa mipango na mikakati ya huduma za afya na ustawi wa jamii umeleta mafanikio katika maeneo mbalimbali hapa nchini kama ifuatavyo: -

(i) Wananchi wameelimishwa juu ya umuhimu wa huduma za afya na kuhamasishwa kutumia huduma hizo, hali ambayo imechochea mahitaji

makubwa kwa kila ngazi na kila sehemu ya nchi;

(ii) Ushirikishwaji wa wananchi katika huduma za afya umewezesha kuongezeka kwa vituo vya Serikali na binafsi na kuchochea mahitaji makubwa ya watumishi na kupanua vyuo ili kuongeza idadi ya wanaojiunga;

(iii) Uwezo, uzoefu na mifumo ya kutoa huduma ya mama na mtoto na ya kukabiliana na magonjwa ya kuambukiza yakiwemo maradhi makuu kama vile malaria, kifua kikuu na UKIMWI umejengwa na kuimarika;

(iv) Sheria mbalimbali zimetungwa na nyingine kufanyiwa mapitio kutokana na mabadiliko katika Sekta ya Afya kwa lengo la kuboresha usimamizi wa huduma za Afya nchini na kulinda afya za wananchi.

### 2.2.2 Upungufu

Pamoja na mafanikio yaliyopatikana, katika utekelezaji wa sera ya 1990 bado kuna upungufu katika kufikia malengo yaliyokusudiwa kama ifuatavyo: -

(i) Sera hiyo haikuweza kuweka mifumo ya kutosheleza mahitaji ya huduma za afya kwa ngazi mbalimbali katika maeneo mengi ya nchi yetu, kwa mfano usambazaji wa dawa, vifaa na vifaa tiba;

(ii) Uhaba wa wataalam wa kada mbalimbali, vifaa, dawa, vitendanishi na vifaa tiba katika sekta ya Afya;

(iii) Kukosekana kwa vivutio maalum kwa wataalam, vya kuwahamasisha kubaki katika vituo vya huduma na maeneo mbalimbali ya nchi;

(iv) Changamoto ya maendeleo na mabadiliko ya tabia na mwenendo wa maisha imebadili sura ya magonjwa. Aidha, hali hii imesababisha kuanza kujitokeza kwa magonjwa ya kuambukiza na yasiyo ya kuambukiza na yanayotokana na ajali na majanga, ambayo kwa huduma zilizopo haziwezi kukidhi;

(v) Wananchi wengi wanaendelea kusumbuliwa na magonjwa ambayo hayakupewa umuhimu, kwa mfano matende, ngirimaji, kichocho na vikope. Wakati huo huo, magonjwa mapya yameanza kujitokeza kwa nguvu, kwa mfumo wa milipuko, mfano; homa ya bonde la ufa, homa ya mafua ya ndege ambapo mfumo wa huduma uliopo haukidhi mahitaji;

(vi) Baadhi ya magonjwa yaliyojitokeza kwa mfano; UKIMWI, yameibua mahitaji maalum katika dhana ya lishe bora na huduma za utengemao.

### 2.2.3 Changamoto

Changamoto ambazo sekta ya afya inakabiliana nazo katika kutoa huduma ni kama ifuatavyo:

(i) Namna ya kuongeza watumishi, ili kukidhi mahitaji ya sekta ya afya katika ngazi zote;

(ii) Jinsi ya kuongeza bajeti ya sekta ya afya katika ngazi zote hadi kufikia kiwango kisichopungua asilimia 15 ya bajeti yote ya Serikali, kama ilivyopitishwa na Azimio la Abuja;

(iii) Kasi ya maambukizi mapya na athari za UKIMWI katika jamii ikizingatiwa kuwa asilimia 7 ya Watanzania wameambukizwa virusi vya UKIMWI;

(iv) Kuhakikisha kuwa vifo vya watoto wachanga, wenye umri chini ya mwaka mmoja, vinapungua zaidi ya 68 kwa watoto 1000 waliozaliwa hai;

(v) Kupunguza viwango vya utapiamlo kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano;

(vi) Kupunguza viwango vya vifo vya wanawake vinavyotokana na uzazi;

(vii) Kupunguza ongezeko kubwa la watoto yatima na walio katika mazingira magumu;

(viii) Kupandisha ari ya utendaji kazi wa watumishi wa sekta ya afya kutokana na mishahara midogo, ukosefu wa motisha na upungufu wa vitendea kazi;

(ix) Kudhibiti athari za utandawazi na kasi ya mabadiliko ya teknolojia ya sayansi ya afya;

(x) Kudhibiti ongezeko kubwa la bei za dawa, vifaa na vifaa tiba;

(xi) Kudhibiti ongezeko la vimelea vya magonjwa kuwa sugu kwa dawa zinazotumika;

(xii) Kudhibiti ongezeko la magonjwa yasiyokuwa ya kuambukiza yakiwemo; kisukari, magonjwa ya moyo, saratani na ajali;

(xiii) Kuzuia kuibuka kwa magonjwa ya kuambukiza yaliyoonekana kudhibitiwa huko nyuma;

(xiv) Kuongeza ushiriki wa wananchi katika usafi wa mazingira, kama njia ya udhibiti wa magonjwa ya kuambukizwa;

(xv) Kupambana na kuzuka kwa magonjwa mapya duniani kama vile; ugonjwa wa Kichaa cha ng'ombe unaoathiri binadamu, homa ya Mafua ya ndege, Ebola na SARS;

(xvi) Kukidhi matarajio ya wananchi kwa kuwa na huduma bora za afya;

(xvii) Udhibiti wa vitendo vya rushwa kwa baadhi ya watumishi wa afya na ubinafsi katika utoaji wa huduma;

(xviii) Utendaji na uwajibikaji unaogongana katika ngazi mbalimbali za kutolea huduma na maamuzi;

(xix) Mfumo thabiti wa kuhudumia wastaafu, wategemezi wao na wazee;

(xx) Kupunguza utegemezi wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi kutoka nje ya nchi;

(xxi) Mfumo madhubuti na endelevu wa kuendeleza watumishi katika sekta ya afya;

(xxii) Usimamizi bora na endelevu wa Sekta binafsi zinazoongezeka kwa kasi nchini;

(xxiii) Kuongezeka kwa ugonjwa wa malaria na usugu wa vimelea vya ugonjwa huo ambao unachangia zaidi ya asilimia 40 ya wagonjwa wote wa nje na asilimia 38 kwa wagonjwa wote wanaolazwa;

## 3.0 UMUHIMU WA SERA

Sera ya mwaka 1990, ambayo imekuwa ikitumiwa hadi sasa haikidhi mahitaji ya sekta ya afya kutokana na mabadiliko yaliyojitokeza na yanayoendelea kujitokeza ya kiuchumi na kijamii, kuongezeka kwa magonjwa mapya na yanayojirudia kama; UKIMWI na Kifua Kikuu, uanzishaji wa utaratibu wa mfumo wa wananchi kuchangia huduma za afya na kuanzishwa kwa utaratibu wa wananchi kuwa na madaraka ya kushiriki katika kutoa maamuzi na kumiliki raslimali za sekta ya afya. Sababu nyingine zilizochangia Sera ya mwaka 1990 kutokidhi mahitaji ya sasa na wakati ujao, ni pamoja na kuwepo kwa maendeleo mapya ya sayansi na teknolojia, utekelezaji wa dira na mikakati ya taifa na utekelezaji wa mikataba ya kimataifa ikiwemo Malengo ya Milenia.

Sera hii iliyopitiwa, inazingatia masuala yote yaliyotajwa hapo juu na pia, ni mwendelezo wa utekelezaji wa malengo yalioanishwa katika Sera ya mwaka 1990. Aidha, Sera hii ni muhimu kwani inatoa maelekezo ya jinsi ya kuanzisha, kuendesha na kutoa huduma za afya nchini kwa lengo la kuhakikisha kwamba kila mtu anapata huduma za afya zilizo bora na zenye uwiano na haki. Serikali inatambua kwamba wananchi walio na afya bora ni raslimali kubwa katika kukuza uchumi na kupunguza umaskini. Aidha, sera inalenga katika kuwezesha ushirikishwaji wa wananchi na wadau katika utoaji wa huduma za afya.

## 4.0 DIRA, MAKUSUDIO NA MADHUMUNI YA SERA

### 4.1 Dira

Kuwa na jamii yenye afya bora na ustawi ambayo itachangia kikamilifu katika maendeleo binafsi na ya nchi.

### 4.2 Makusudio

Kutoa huduma muhimu za afya zenye uwiano wa kijiografia, viwango vya ubora unaokubalika, gharama nafuu na zilizo endelevu.

### 4.3 Madhumuni

Kuinua hali ya afya ya wananchi wote na hasa wale walioko kwenye hatari zaidi, kwa kuweka mfumo wa huduma za Afya utakaokidhi mahitaji ya wananchi na kuongeza umri wa kuishi wa watanzania.

#### 4.3.1 Madhumuni mahsusi

(i) Kupunguza magonjwa na vifo, ili kuongeza umri wa kuishi wa watanzania wote kwa kutoa huduma bora za afya, pamoja na kuzingatia mahitaji ya makundi maalum, hususan; watoto wachanga na walio chini ya umri wa miaka mitano, watoto walio katika umri wa kuanza shule na walio shuleni, vijana, watu wenye ulemavu, wanawake walio katika umri wa uzazi na wazee.

(ii) Kuhakikisha kuwa huduma za afya ya msingi zinapatikana na kutolewa na mfumo madhubuti na kushirikisha jamii, kwa kuzingatia sheria na miongozo iliyopo.

(iii) Kukinga na kudhibiti magonjwa ya kuambukiza na yale yasiyo ya kuambukiza, hususan; Virusi vya UKIMWI na UKIMWI, Malaria, Kifua Kikuu, magonjwa yatokanayo na lishe duni, afya ya mazingira, na sehemu za kazini na usimamizi wa kemikali.

(iv) Kuhamasisha wananchi kuhusu maradhi yanayoweza kuzuilika, ili waweze kuyatambua na kutafuta mbinu za kuyadhibiti.

(v) Kumuelimisha kila mwananchi, aelewe kuwa anawajibika moja kwa moja kutunza afya yake na ile ya familia yake.

(vi) Kujenga ushirikiano kati ya sekta ya umma, sekta binafsi, mashirika ya dini, asasi za kijamii na jamii katika kutoa huduma za afya.

(vii) Kupanga, kutoa mafunzo na kuongeza idadi ya wataalam wa afya , wenye taaluma inayokidhi viwango kwa kuzingatia usawa wa kijinsia ili kutoa huduma za afya kwa jamii katika ngazi zote.

(viii) Kuainisha, kukarabati miundombinu kwa kuzingatia mahitaji ya watu wenye ulemavu, na kuweka mfumo wa kukarabati vituo vya kutolea huduma za afya, vifaa na vitendea kazi.

(ix) Kufanya mapitio na kutathmini Sera ya Afya, Miongozo, Sheria na viwango vya utoaji huduma za afya.

## 5.0 HOJA ZA SERA NA MATAMKO

Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa kushirikiana na wadau wengine, ina jukumu la kuinua hali ya afya na ustawi kwa wananchi wote, kwa kuzuia au kupunguza maradhi, ulemavu na vifo na kuwa na afya thabiti kimwili, kiakili na kijamii.

Ili kufikia azma hiyo, Wizara inalo jukumu la kuandaa sera, miongozo na mapendekezo ya sheria zitakazosaidia utoaji na usimamizi wa huduma za uboreshaji afya (Promotive), kinga, tiba na utengamao. Pia, maendeleo ya wataalam wa afya, upatikanaji na usimamizi wa raslimali watu, fedha, vifaa, miundombinu, mipango bora ya afya, yenye viwango vinavyo kubalika na zinazowafikia wananchi wote. Aidha, Wizara ina jukumu la kuboresha mahusiano na ushirikiano na sekta binafsi, mashirika ya kimataifa na wadau mbalimbali wa maendeleo katika utoaji wa huduma za afya.

Sera hii inatoa maelezo, madhumuni na matamko ya suala kuhusu utoaji wa huduma za afya nchini katika kila eneo muhimu la huduma za afya kama ifuatavyo: -

### 5.1 Afya ya Msingi

#### (a) Maelezo

Mkakati wa Afya ya msingi ulilenga kuimarisha afya za wananchi kuanzia ngazi ya kaya, hadi taifa kwa kuwashirikisha wananchi wenyewe. Mkakati huu ulilenga kuwezesha upatikanaji wa huduma muhimu za afya kwa wananchi wote na ulitoa kipaumbele katika uboreshaji afya, kinga na tiba. Maeneo yaliyozingatiwa katika uboreshaji wa afya ni elimu ya afya, uhamasishaji wa lishe bora, afya ya mazingira na afya mashuleni; kinga ni huduma za mama na mtoto, chanjo dhidi ya magonjwa ya kuambukiza na tiba ni matibabu kwa maadili ya kawaida na majeraja, dawa muhimu, huduma ya afya ya akili, kinywa na macho.

Tanzania ilikuwa nchi mojawapo duniani ambayo ilitekeleza huduma za afya ya msingi kwa mafanikio makubwa sana baada ya uhuru. Uhamasishaji na ushirikishwaji wa wananchi katika kutambua na kujitatulia matatizo yao ya afya uliimarika na kuwa mfano kwa nchi nyingine katika bara la Afrika.

Hata hivyo, kutokana na mabadiliko ya kiuchumi, uwezo wa Serikali na ule wa wananchi wa kuchangia katika huduma hii muhimu umepungua sana na

kusababisha kuenea kwa magonjwa ya mlipuko kama; kipindupindu, kuhara, homa ya matumbo ambayo kwa kiasi kikubwa yanasababishwa na kuzagaa kwa uchafu katika jamii, umeibua hoja ya kuipanua dhana ya afya ya msingi, ili iweze kukidhi mahitaji ya wakati uliopo na ujao.

**(b) Madhumuni**

Kupanua dhana ya afya ya msingi na kuwa na huduma bora za afya zinazoendana na wakati, endelevu na zinazowafikia wananchi wote.

**(c) Tamko la sera**

(i) Serikali itashirikisha wananchi na sekta mbalimbali katika kuimarisha huduma za afya katika ngazi zote ili kuboresha afya.

(ii) Serikali itaimarisha uendeshaji na usimamizi wa huduma za afya.

(iii) Serikali itaimarisha mfumo uliopo wa kuongeza umiliki na sauti ya wananchi katika utoaji wa huduma za afya.

(iv) Serikali kwa kushirikiana na wananchi na wadau wengine kwa ujumla itaweka mazingira mazuri ya kuwezesha jamii kubuni njia na mikakati mbalimbali ya kuboresha afya yao.

(v) Serikali itatoa maelekezo kwa kamati za Mamlaka za Serikali za Mtaa ili itekeleze na kusimamia huduma za afya ya msingi katika maeneo yao.

## 5.2 Uboreshaji na Udumishaji wa Afya

Huduma za afya kwa njia ya elimu, uhamasishaji na uragibishi zitaimarishwa na kuboreshwa katika ngazi zote na kipaumbele kitatolewa katika masuala ya lishe na mazingira.

### 5.2.1 Elimu ya afya

**(a) Maelezo**

Elimu ya afya na uhamasishaji ni njia mojawapo muhimu katika utoaji wa huduma za afya. Njia hii inatumia utaalamu wa mawasiliano na kutayarisha na kuwasilisha ujumbe mbalimbali kwa mtu binafsi, familia na jamii kwa lengo

la kubadilisha mienendo na tabia zinazochangia kuwepo au kutokuwepo kwa maradhi katika jamii. Mbinu mbalimbali kama vyombo vya habari, mabango, vipeperushi, majarida, vitabu na wavuti hutumika kushawishi na kuwasilisha ujumbe huo. Katika utekelezaji wa elimu ya afya na uhamasishaji, serikali imefanikiwa kutoa elimu ya afya kwa wananchi pamoja na kuwahamasisha namna ya kuzuia magonjwa ya kuambukiza. Magonjwa mengi yamedhibitiwa, hasa yale yanayoweza kuzuilika kwa chanjo.

Hata hivyo, elimu ya afya inayotolewa bado haijaleta mabadiliko makubwa ya tabia na mienendo inayotarajiwa katika jamii. Aidha, mazingira yaliyopo kuanzia ngazi ya kaya hadi taifa hayatoshelezi kila mtu kuweza kukuza, kulinda na kuendeleza afya yake.

**(b) Madhumuni**

Kuweka mazingira mazuri yatakayowezesha kila mtu kulinda na kuendeleza afya yake kwa ufanisi.

**(c) Tamko la sera**

(i) Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali itaimarisha utoaji wa elimu ya afya, ili kumhamasisha na kumwezesha kila mtu kujenga tabia inayozingatia kanuni za afya na maisha bora.

(ii) Serikali kwa kushirikiana na wadau itaandaa sheria, miongozo na mikakati ambayo itakayowezesha kila mtu kupata elimu, ili kulinda, kukuza na kuendeleza afya bora.

### 5.2.2 Uhamasishaji na Ushirikishaji

**(a) Maelezo**

Uhamasishaji na ushirikishaji ni mbinu inayotumika katika kushawishi mtu mmoja mmoja, makundi na jamii kwa ujumla kuhusu umuhimu wa kushiriki katika kulinda, kuendeleza na kudumisha afya bora. Tangu uhuru, Serikali imeendelea kutumia uhamasishaji kama mbinu muhimu ya kuwafanya watu kubadili tabia, ili waweze kufuata kanuni bora za afya na kulinda afya zao. Uhamasishaji huu unajikita zaidi katika masuala muhimu ya afya, ambayo ni pamoja na; elimu ya afya kwa umma, lishe bora, ushirikishwaji jamii na usafi wa mazigira.

Baadhi ya mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na; udhibiti wa magonjwa, watu wengi wamehamasika kuhusu afya zao na kuchangia kikamilifu katika

kupambana na magonjwa ya milipuko kwa kuweka mazingira safi, kutumia maji yaliyochemshwa, kutunza afya binafsi, kuepuka tabia mbaya ya kuvuta sigara, kutumia chumvi iliyowekwa madini na uchimbaji, pamoja na kutumia vyoo.

Hata hivyo, pamoja na mafaniko hayo uhamasishaji wa wananchi katika kudumisha afya bora na endelevu katika jamii ni wa kiwango cha chini. Magonjwa ya milipuko pamoja na uchafuzi wa mazingira yameendelea kuwepo.

Aidha, viwango vya utapiamlo katika jamii viko juu pamoja na ushiriki wa wananchi katika masuala ya afya kuwa ni kiwango cha chini. Kwa hiyo, juhudi zaidi za uhamasishaji zinapaswa kuchukuliwa, ili wananchi waweze kulinda na kudumisha afya bora na endelevu.

**(b) Madhumuni**

Kuhamasisha jamii, ili iweze kuweka mazingira yatakakayowezesha kila mtu kulinda, kuendeleza na kudumisha afya bora, ikiwa ni pamoja na; lishe bora na kuweka mazingira katika hali bora na endelevu.

**(c) Tamko la sera**

(i) Serikali kwa kushirikisha wadau mbalimbali itaimarisha utoaji wa elimu ya afya, ili kumhamasisha na kumwezesha kila mtu kujenga tabia inayozingatia kanuni za afya na maisha bora.

(ii) Serikali kwa kushirikiana na wadau, itaandaa na kusimamia sheria, miongozo, kanuni na mikakati ya afya, lishe na usafi wa mazingira ambayo itamwezesha kila mtu kulinda, kutunza na kuendeleza afya yake.

(iii) Serikali itaweka na kusimamia viwango vya lishe.

(iv) Serikali kwa kushirikiana na wadau wengine itahamasisha ushiriki wa wananchi katika masuala yote yanayohusu afya, ikiwa ni pamoja na; kupanga, kutekeleza, kusimamia na kutathmini huduma za afya katika jamii zao.

### 5.2.3 Afya ya Mazingira

**(a) Maelezo**

Afya ya mazingira ni majumuisho ya juhudi mbalimbali zinazotumika katika kuweka makazi na sehemu za kazi pamoja na mandhari katika hali ya usafi. Asilimia kubwa ya magonjwa mengi yanayoathiri afya ya jamii yanatokana na uduni na uchafuzi wa mazingira na tabia duni za kiafya. Katika kukabiliana

na hali hii, elimu na kampeni mbalimbali zimekuwa zikitolewa kwa wananchi wote kwa kutumia mbinu mbalimbali. Halmashauri nyingi za miji zinasimamia utekelezaji wa usafi wa mazingira. Aidha, kumekuwepo na kupungua kwa maradhi ya milipuko katika baadhi ya maeneo nchini.

Pamoja na juhudi hizi, bado kuna upungufu katika mfumo wa kulinda na kuimarisha afya ya mazingira pamoja na kuwa na maeneo ya mazishi. Maeneo ambayo yamekuwa na upungufu mkubwa ni pamoja na; kutokuwepo kwa vyoo bora vinavyokidhi mahitaji ya kiafya, udhibiti duni wa taka ngumu na taka maji zitokanazo na huduma ya afya, ushiriki duni wa jamii na sekta binafsi, pamoja na uchafuzi wa mazingira unaosababisha kuzaliana kwa wadudu na wanyama wanaoleta maradhi.

**(b) Madhumuni**

Kulinda afya ya jamii kwa kuboresha usafi wa mazingira ulio endelevu.

**(c) Tamko la sera**

(i) Serikali kwa kushirikiana na wadau itahakikisha jamii inazingatia kanuni za usafi wa mazingira.

(ii) Serikali itaimarisha mfumo wa utupaji na uteketezaji salama wa taka zitokanazo na huduma ya afya, ikiwa ni pamoja na; dawa, vifaa, vifaa tiba, kemikali na vitendanishi vya maabara vilivyoharibika au kuisha muda wake.

(iii) Kwa kushirikiana na Halmashauri za miji na wadau wengine Serikali itasimamia utaratibu na ubora wa maeneo yanayokidhi mahitaji ya mazishi

### 5.2.4 Afya kazini

Wizara inatambua uwepo wa Wakala wa Serikali wa kusimamia usalama na afya ya wafanyakazi ambao wamepewa jukumu la kusimamia afya na usalama wa wafanyakazi kazini. Aidha, wizara itaendelea kushirikiana kwa karibu na wakala hao.

### 5.2.5 Lishe

**(a) Maelezo**

Lishe ni majumuisho ya hatua mbalimbali tokea chakula kinapoliwa na jinsi

miili yetu inavyochukua virutubisho na kuvitumia katika kumpatia mlaji afya bora. Lishe bora kutokana na ulaji unaofaa, yaani; chakula cha kutosha, na cha mchanganyiko chenye virutubishi katika uwiano unaotakiwa. Lishe duni hasababisha utapiamlo ambao huleta madhara ya kiafya.

Serikali imetakiwa kuweka msisitizo katika kuboresha lishe na afya za wananchi wake. Hata hivyo, juhudi za Serikali za kuhamasisha na kuelimisha jamii umuhimu wa lishe bora bado hazijapata mafanikio ya kuridhisha. Viwango vya utapiamlo bado viko juu. Hali hii, inahitaji juhudi zaidi, ili tupunguze utapiamlo katika jamii.

**(b) Madhumuni**

Kuimarisha na kuboresha huduma za lishe nchini.

**(c) Tamko la sera**

(i) Serikali itaweka mazingira mazuri kwa wadau kushiriki katika kuboresha huduma za lishe

## 5.3 Kinga

### 5.3.1 Udhibiti wa magonjwa

**(a) Maelezo**

Kinga ni njia kuu ya huduma za afya inayotumika katika kuzuia magonjwa yasitokee katika jamii. Tangu Uhuru nchi ya Tanzania imetilia mkazo zaidi kinga na kuzingatia usemi unaosema Kinga ni bora na rahisi kuliko tiba. Kwa kutumia njia hii magonjwa mengi ya kuambukiza katika jamii kwa mfano; Kipindupindu, kuhara damu, surua, homa ya uti wa mgongo na ugonjwa wa kupooza yaliweza kupungua kwa kiasi kikubwa.

Aidha, baadhi ya magonjwa yalitokomezwa kabisa kwa mfano ndui. Hata hivyo, bado kuna magonjwa yaliyopo na magonjwa mapya yanayoibuka na yanayojirudia ambayo husababisha vifo na ulemavu. Kwa hiyo jitihada zaidi zinahitajika ili kuweza kudhibiti hali hii na kuwezesha jamii kuwa na afya njema.

**(b) Madhumuni**

Kuimarisha ubora na ufanisi katika utoaji wa huduma za kinga ili kuzuia maradhi na ulemavu na hivyo kupunguza vifo na gharama za kutibu magonjwa.

**(c) Tamko la sera**

(i) Serikali kwa kushirikiana na jamii na wadau wengine itaimarisha huduma za kinga zilizo na ubora, zinazojitosheleza na kutolewa kwa usawa na uwiano.

(ii) Serikali itaimarisha na kudumisha mazingira mazuri, ili wananchi waweze kulinda na kutunza afya zao, kwa kuzingatia miongozo mbalimbali ya stadi za maisha na afya ya mazingira.

(iii) Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali na mashirika ya kimataifa itaimarisha udhibiti na uzuiaji wa magonjwa, hasa yale yanayoweza kuingizwa kutoka nje ya nchi kupitia bandarini na mipakani.

(iv) Serikali kwa kushirikiana na wadau itaweka utaratibu wa kuchunguza na kutibu magonjwa yasiyo ya kuambukiza na ajali katika ngazi zote.

### 5.3.2 Magonjwa ya kuambukiza na milipuko

**(a) Maelezo**

Magonjwa ya kuambukiza kama vile UKIMWI, Kifua kikuu, malaria, mengineyo pamoja na milipuko kama vile kipindupindu, tauni na surua yanaendelea kuwa ni tatizo la kiafya kwa jamii katika nchi. Aidha, magonjwa mapya na yale yanayojirudia kama vile, Ebola, Mafua ya ndege, Homa ya Bonde la Ufa na Kifua Kikuu yameongezea tatizo.

Jitihada kubwa imetumika katika kudhibiti na kupambana na magonjwa haya, kwa kutumia mbinu mbalimbali kama vile; kutoa elimu ya afya na uhamasishaji kwa umma, kuimarisha huduma za chanjo pamoja na kampeni, kuelimisha watumishi, kuimarisha utambuzi na tiba pamoja na ufuatiliaji wa wagonjwa. Hata hivyo, pamoja na jitahada hizi, bado magonjwa ya kuambukiza, magonjwa ya milipuko, mapya na yanayojirudia yanaendelea kuwa tatizo kubwa la kiafya kwa jamii.

**(b) Madhumuni**

Kuimarisha, kubuni na kuboresha mbinu mbalimbali za kudhibiti na kuzuia magonjwa ya kuambukiza, milipuko na magonjwa yanayojirudia na mapya ili kupunguza kwa kiasi kikubwa maradhi na vifo.

**(c) Tamko la sera**

(i) Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali zikiwemo jumuiya za kimataifa itaendelea kuandaa na kuboresha sheria, miongozo na mikakati ya kudhibiti magonjwa ya kuambukiza, milipuko pamoja na yale yanayojirudia na mapya kwa wakati muafaka.

(ii) Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi, mashirika ya kimataifa, taasisi zinazotoa huduma bila faida itahakikisha upatikanaji wa; chanjo, dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi vya kutosha kwa ajili ya kudhibiti magonjwa ya kuambukiza ya milipuko.

(iii) Serikali itashirikisha jamii na wadau wengine katika kuimarisha na kuboresha mfumo wa utoaji huduma za kinga ikiwa ni pamoja na; programu maalumu na mbinu za kuleta matokeo yanayotarajiwa katika kuzuia na kudhibiti magonjwa ya kuambukiza.

(iv) Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi, mashirika ya kimataifa, taasisi zinazotoa huduma bila faida itaendelea; kusimamia, kufuatilia, kuweka takwimu sahihi zonazotosheleza na kuratibu matokeo ya tafiti na matumizi yake kuhusu magonjwa ya kuambukiza na milipuko yanayojirudia na mapya.

(v) Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi, mashirika ya kimataifa, taasisi zinazotoa huduma bila faida, itaimarisha uwezo kwa watumishi kwa ajili ya kudhibiti magonjwa ya kuambukiza, milipuko na utayari wa kukabiliana na maafa yatokanayo na milipuko.

### 5.3.3 Magonjwa yasiyo ya kuambukiza na ajali

**(a) Maelezo**

Mwenendo wa magonjwa sugu au yasiyo ya kuambukiza na majeraha yanayosababishwa na ajali mbalimbali unaongezeka kwa kasi. Magonjwa ni; kisukari, magonjwa ya moyo, magonjwa yatokanayo na lishe duni, saratani, magonjwa ya akili na ajali zinazosababishwa na sumu mbalimbali, kujinyonga, ajali kazini na vyombo vya usafiri, mafuriko na tetemeko.

Juhudi mbalimbali zimechukuliwa na Serikali katika kukabiliana na hali hii, kwa mfano; kumarisha utambuzi wa vituo vya tiba, kutoa elimu kwa wataalam, kuimarisha mpango wa kukabiliana na majanga pamoja na kuelimisha jamii juu

ya udhibiti magonjwa, majanga na hali zonazojitokeza. Hata hivyo, mafanikio bado yamekuwa hafifu kutokana na upungufu wa miundombinu na gharama kubwa zinazohitajika katika kukabili hali hiyo.

**(b) Madhumuni**

Kubuni, kuboresha na kuimarisha mbinu mbalimbali za kubadilisha tabia na maisha potofu kwa watu na jamii, ili kuzuia na kudhibiti magonjwa sugu na yasiyo ya kuambukiza na majeraha na kupunguza athari zinazosababishwa na ajali mbalimbali.

**(c) Tamko la sera**

(i) Serikali itaandaa miongozo na mikakati ya kushirikisha jamii katika kudhibiti magonjwa sugu na yasiyo ya kuambukiza.

(ii) Serikali itaimarisha ushiriki wa sekta mbalimbali za umma na za binafsi katika kukabiliana na vyanzo vinavyosababisha magonjwa yasiyo ya kuambukiza na ajali.

(iii) Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi, mashirika ya kimataifa, taasisi zinazotoa huduma bila faida itaendelea; kuandaa na kurekebisha sheria, kanuni na taratibu zitakazoimarisha uzuiaji na udhibiti wa magonjwa yasiyo ya kuambukiza pamoja na ajali.

(iv) Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi, mashirika ya kimataifa, taasisi zinazotoa huduma bila faida itaendelea; kusimamia na kuratibu tafiti kuhusu magonjwa yasiyo ya kuambukiza na ajali.

(v) Kwa kushirikiana na asasi mbalimbali, Serikali itaimarisha mfumo wa usafirishaji majeruhi ili kuzuia athari zinazotokana na ajali.

### 5.3.4 Afya ya Mama na Mtoto

**(a) Maelezo**

Afya ya mama na mtoto ni mfumo wa utoaji huduma maalum kwa wanawake walio katika umri wa uzazi na watoto wenye umri chini ya miaka mitano, hasa watoto wachanga tangu kuzaliwa hadi siku 28. Huduma hizi zinajumuisha kutambua vidokezo hatari kwa wanawake na watoto, chanjo, tiba, elimu ya uzazi, uzazi salama, mbinu shirikishi za udhibiti wa magonjwa ya watoto, afya katika jamii, lishe na afya shuleni.

Juhudi kubwa zimefanyika na Serikali kwa kushirikiana na wananchi na

wadau mbalimbali katika kupanua, kuboresha na kusambaza huduma hizo kwa walengwa. Aidha, huduma za chanjo na mnyororo baridi zimeonyesha mafanikio makubwa na kuifanya nchi yetu kupata medali ya kimataifa na kuwa mfano wa kuigwa katika bara la Afrika.

Hata hivyo, pamoja na mafanikio hayo, bado vifo vya wanawake wajawazito na watoto wachanga vimeendelea kuwa juu. Kiwango cha vifo vya wanawake kimeongezeka kutoka 529 mwaka 1996 hadi kufikia 578 mwaka 2005 kwa kila watoto 100,000 waliozaliwa hai.

Kutokana na hali hiyo upo umuhimu wa kuongeza juhudi katika utoaji wa huduma hii ili kupunguza vifo vya wanawake wajawazito na watoto wachanga kwa kiasi kikubwa.

**(b) Madhumuni**

Kupunguza kwa kiasi kikubwa vifo na athari za magonjwa kwa wanawake wajawazito, pamoja na watoto wenye umri chini ya miaka mitano hasa watoto wenye umri chini ya mwaka mmoja kulingana na Malengo ya Milenia.

**(c) Tamko la sera**

(i) Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi inayotoa huduma bila faida, na mashirika ya kimataifa, itaendelea kutoa huduma bila malipo kwa; wanawake wajawazito, watumiaji wa huduma za uzazi wa mpango na watoto wenye umri chini ya miaka mitano.

(ii) Serikali kwa kushirikiana na wadau itaandaa na kusimamia utekelezaji wa miongozo, mikakati na mipango endelevu ya kupunguza vifo vya wanawake vinavyotokana na uzazi pamoja na vifo vya watoto wenye umri chini ya miaka mitano hasa watoto wachanga.

(iii) Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali na wananchi itaboresha miundo mbinu ili kuwawezesha; wanawake wajawazito na watoto wachanga kufikiwa na kutumia huduma za afya.

(iv) Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali itaendelea kuhamasisha na kuelimisha wananchi hasa wanawake kuhusu umuhimu wa huduma za afya.

### 5.3.5 Afya ya Uzazi

**(a) Maelezo**

Afya ya uzazi ni huduma inayotolewa kwa wanawake, wanaume na vijana walio katika umri wa kuzaa. Huduma hii inajumuisha magonjwa ya uzazi yanayohusisha; kupanga uzazi, ujauzito, magonjwa ya kujamiiana, ukeketaji na mila potofu, saratani ya via vya uzazi, kuzuia na kutibu ugumba. Huduma ya afya ya uzazi imeendelea kuboreshwa nchi nzima kwa kiwango cha kuridhisha. Makundi mbalimbali yanashiriki katika kupata huduma hizi katika vituo vya kutolea huduma.

Hata hivyo, kutokuwepo kwa elimu na uhamasishaji wa kutosha wa afya ya uzazi kwa makundi mbalimbali na hasa vijana na wanaume kumesababisha kuongezeka kwa magonjwa ya ngono pamoja na matatizo ya mimba zisizotarajiwa, hasa maeneo ya vijijini. Pia, mila potofu zimechangia katika kuzorotesha afya ya uzazi katika baadhi ya maeneo.

**(b) Madhumuni**

Kuboresha huduma ya afya ya uzazi kwa makundi yote na hasa; wanaume, vijana na watu wenye ulemavu ambao wamekuwa hawashiriki kikamilifu.

**(c) Tamko la sera**

(i) Serikali itashirikiana na wadau mbalimbali kuimarisha afya ya uzazi ya wanawake na wanaume, watu wenye ulemavu, vijana na wazee.

(ii) Serikali itaandaa miongozo, mikakati na kuratibu shughuli zinazolenga afya ya uzazi ya makundi mbalimbali pamoja na kuhakikisha huduma za uzazi wa mpango unatekelezwa.

(iii) Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali itahakikisha utoaji wa huduma bora za uzazi katika vituo vya kutolea huduma za afya zinazowavutia wanawake, wanaume na vijana.

## 5.4 Tiba

**(a) Maelezo**

Serikali ina jukumu la kusimamia huduma za afya nchini katika vituo vya umma, mashirika ya dini, mashirika yasio ya kiserikali na watu binafsi. Aidha, tiba inatakiwa kuwa salama kulingana na mahitaji ya wagonjwa na kwa uwiano. Ili kufikia azma hii, kila ngazi inatakiwa kuwa na wataalam, majengo na vifaa kulingana na mwongozo wa majukumu ya ngazi husika. Vilevile, wagonjwa

wanatakiwa kupata rufaa kutoka ngazi moja kwenda nyingine kulingana na matatizo na uwezo wa kituo cha huduma za afya.

Hali halisi ni kwamba huduma za tiba, utengamao na mfumo wa rufaa hazitoshelezi mahitaji ya wagonjwa katika ngazi zote za utoaji huduma. Hali hii imesababisha malalamiko kutoka kwa wananchi na wagonjwa wengi kulazimika kupata rufaa nje ya nchi kutokana na ukosefu wa wataalam na vifaa nchini.

**(b) Madhumuni**

Kuimarisha mfumo wa utoaji huduma za afya, utaratibu wa rufaa, upatikanaji wa wataalam na vifaa ili kuboresha huduma za afya zilizo sahihi, salama, uwiano na endelevu.

**(c) Tamko la sera**

(i) Serikali itasimamia sheria, kanuni, taratibu na miongozo ya mfumo, muundo na rufaa ya utoaji tiba kuanzia ngazi ya zahanati, kituo cha afya hadi hospitali za ngazi mbalimbali.

(ii) Serikali kwa kushirikiana na wadau itahakikisha kuwa kila kijiji kina zahanati na kila kata ina kituo cha afya ili kuleta uwiano katika utoaji wa huduma za afya kwa wananchi.

(iii) Serikali kwa kushirikiana na wadau itaimarisha mfumo wa rufaa nchini ili kuboresha matumizi ya wataalam na raslimali kwa lengo la kupunguza idadi, aina na gharama za kutibu wagonjwa nje ya nchi.

(iv) Serikali kwa kushirikiana na wadau itaimarisha huduma za tiba ngazi ya kaya kwa magonjwa sugu na yenye kuhitaji matibabu ya muda mrefu.

(v) Serikali kwa kushirikiana na wamiliki wa vituo vya kutolea huduma za afya itaimarisha usimamizi unaofanywa na Bodi na Kamati katika ngazi mbalimbali.

(vi) Serikali itaweka mazingira mazuri ya kushirikisha jamii kuimarisha huduma za utambuzi wa awali na utengamao unaosababishwa na magonjwa mbalimbali na ajali.

### 5.4.1 Mfumo wa utoaji huduma za afya kwa uwiano wa kijiografia

**(a) Maelezo**

Ni mfumo wa rufaa unaotoa huduma za afya kuanzia ngazi ya zahanati , vituo vya afya na hospitali ili kuhakikisha kila mtu anapata huduma za afya karibu na eneo analoishi. Katika mfumo huu, zahanati zilipangwa kujengwa umbali wa kilometa 5 za mduara na kilometa 10 za mduara kwa kila kituo cha afya, hospitali katika kila wilaya, mkoa na pia hospitali za rufaa na maalum.

Mafanikio ya utaratibu huu, ni kuwa na idadi kubwa ya zahanati, vituo vya afya, hospitali maalum na hospitali za rufaa zenye mpangilio mzuri wa kutoka ngazi ya kijiji hadi ngazi ya Taifa. Hata hivyo, kutokana na nchi yetu kuwa kubwa, kuongezeka kwa idadi ya watu, upungufu mkubwa wa wafanyakazi na vitendea kazi, ufinyu wa bajeti, umbali mrefu wa kufikia huduma za afya umesababisha lengo la kuongeza uwiano wa upatikanaji wa huduma za afya lisifikiwe kama ilivyotarajiwa. Juhudi zitaendelea kufanyika ili kuhakikisha kuwa wananchi wanapata huduma za afya karibu na maeneo wanayoishi.

**(a) Madhumuni**

Kuwa na mfumo madhubuti na endelevu wa utoaji huduma, unaozingatia uwiano na usawa katika upatikanaji wa huduma za afya karibu na maeneo wanayoishi wananchi wote.

**(b) Tamko la sera**

(i) Serikali itaendelea kusogeza huduma za afya karibu na wananchi kwa kuwa na zahanati kwa kila kijiji na kituo cha afya kwa kila kata na hospitali kwa kila wilaya, hospitali ya rufaa kila mkoa na hospitali maalum ngazi ya taifa kwa kushirikiana na wananchi na wadau wote kwa ujumla.

(ii) Serikali itaandaa na kupitia miongozo inayosimamia mfumo wa utoaji wa huduma za afya kwa uwiano kwa kuzingatia mahitaji ya makundi maalum.

(iii) Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi itaweka utaratibu utakaowezesha kupatikana kwa watumishi wa kutosha na wenye ujuzi unaotakiwa.

(iv) Serikali itaimarisha huduma za rufaa nchini kwa kupandisha ngazi

hospitali za mkoa kuwa daraja la pili za rufaa na hospitali za wilaya kuwa daraja la kwanza.

(v) Serikali itasimamia upatikanaji wa dawa, vifaa na vifaa tiba, samani pamoja na mitambo husika katika vituo vya kutolea huduma za afya .

(vi) Serikali itaweka na kusimamia viwango kwa majengo yote ya kutolea huduma za afya na kuimarisha utaratibu wa mahusiano na watoa huduma wote.

(vii) Serikali kwa kushirikiana na wadau na wananchi itaendeleza juhudi zake za kupanua na kukarabati majengo ya kutolea huduma za afya.

(viii) Serikali itahakikisha kuna uwiano kijiografia katika kutoa huduma za afya hapa nchini.

### 5.4.2 Uuguzi na Ukunga

#### (a) Maelezo

Huduma za uuguzi na ukunga zinatolewa katika mfumo uliopo kwenye ngazi mbalimbali za huduma za afya nchini. Uuguzi na ukunga ni muhimu katika kupunguza maumivu kwa wagonjwa, kuboresha huduma za mama na mtoto na makundi mengine ya jamii.

Huduma za uuguzi na ukunga zimezoeleka kwamba zinatolewa katika mazingira ya zahanati, vituo vya afya na hospitali tu za umma na binafsi. Hali halisi ni kuwa huduma hizo sasa zinatolewa pia nje ya vituo hivyo katika kaya na jamii. Hali hii imetokana na kuwepo kwa ongezeko la magonjwa sugu yanayohitaji tiba na matunzo ya muda mrefu, mahitaji ya huduma za utengemao na umuhimu wa ushirikishwaji wa jamii katika upangaji na utoaji wa huduma za afya.

Hivyo, wigo na ubora wa huduma za uuguzi na ukunga unahitaji kuinuliwa ili kukidhi matarajio ya wananchi, uwiano, viwango, usalama.

#### (b) Madhumuni

Kuimarisha ubora na usalama wa huduma za uuguzi na ukunga nchini kwa kuzingatia masharti na viwango vya huduma bora na mahitaji ya wananchi.

**(c) Tamko la Sera**

(i) Serikali kwa kushirikiana na wadau itaboresha mazingira ya utoaji wa huduma za uuguzi na ukunga katika sekta za umma na binafsi.

(ii) Serikali kwa kushirikiana na wadau itaimarisha huduma za utengamao kuanzia katika vituo vya huduma hadi katika kaya na jamii.

### 5.4.3 Dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi

**(a) Maelezo**

Upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi ni muhimu katika utoaji wa huduma za afya. Aidha, upatikanaji wake ni moja ya vivutio kwa wananchi kwenda katika vituo vya kutolea huduma za afya.

Pamoja na jitihada za Serikali za kuhakikisha kwamba, dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi vinapatikana, bado kuna upungufu na matatizo ya upatikanaji wake katika vituo vya kutolea huduma za afya na hivyo kuathiri utoaji wa huduma bora.

**(b) Madhumuni**

Kuhakikisha kwamba dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi vinapatikana wakati wote, kwa kiasi cha kutosha na ubora unaotakiwa.

**(c) Tamko la sera**

(i) Serikali kwa kushirikiana na wadau itaimarisha mfumo wa upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi kwa kuzingatia ubora na mahitaji ya nchi.

(ii) Watengenezaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi watawekewa mazingira mazuri ya uzalishaji hapa nchini.

(iii) Mfumo wa matunzo na matengenezo ya vifaa vya kutolea huduma za afya utaimarishwa.

(iv) Serikali itaendelea kuimarisha utengenezaji na upatikanaji wa vifaa vya utengemao na kwa bei nafuu.

### 5.4.4 Uchunguzi wa magonjwa kwa njia ya maabara na radiolojia

**(a) Maelezo**

Uchunguzi wa magonjwa ni kiungo muhimu katika utoaji wa huduma za kinga, tiba na utengemao. Hivyo, uimarishaji wa uchunguzi wa magonjwa ni moja ya nguzo muhimu katika utoaji wa huduma za afya. Hata hivyo, pamoja na juhudi za Serikali kuimarisha huduma za uchunguzi wa magonjwa na vyanzo vya vifo kutokana na makosa ya jinai au mauaji bado hazijafikia kiwango cha kuridhisha na hivyo zinahitaji kuimarishwa.

**(b) Madhumuni**

Kuwa na huduma bora na za kisasa za uchunguzi wa magonjwa na vyazo vya vifo.

**(c) Tamko lo Sera**

(i) Serikali kwa kushirikiana na wadau itaimarisha huduma za uchunguzi wa magonjwa na vyanzo vya vifo.

(ii) Serikali itaimarisha uhakiki wa huduma za uchunguzi wa magonjwa na vifo.

(iii) Serikali kwa kushirikiana na wadau itaimarisha upatikanaji wa vifaa vya maabara, radiolojía na vitendanishi.

(iv) Serikali kwa kushirikiana na wadau itaimarisha mfumo wa matengenezo na huduma kinga ya vifaa vya maabara na radiología.

### 5.4.5 Afya ya Kinywa

**(a) Maelezo**

Afya ya kinywa ni sehemu muhimu katika afya ya jamii. Watanzania wengi wana magonjwa na matatizo mbalimbali katika vinywa vyao. Magonjwa ya kinywa yaliyo mengi yanaweza kuzuilika kwa kuzingatia taratibu za afya. Aidha, magonjwa ya meno yameongezeka kutokana na mabadiliko ya mfumo wa maisha na vyakula. Magonjwa ya Saratani, UKIMWI na maji yenye madini ya florini yanaathiri afya ya kinywa ya wananchi walio wengi.

Hivi sasa, Serikali inatoa huduma za afya ya kinywa kwa wananchi ngazi za wilaya, mkoa na taifa. Hata hivyo, huduma hizi hazijawafikia wananchi walio wengi hususan wanaoishi vijijini. Aidha, huduma zinazotolewa za sasa

hazikidhi mahitaji kutokana na mabadiliko ya teknolojia ya afya ya kinywa.

**(b) Madhumuni**

Kuwa na huduma za afya ya kinywa zilizo bora na za kisasa zinazokidhi mahitaji ya wananchi.

**(c) Tamko la Sera**

(i) Serikali itaandaa kanuni, miongozo na taratibu za utoaji huduma za afya ya kinywa.

(i) Serikali kwa kushirikiana na wadau itapanua huduma za afya ya kinywa sanjari na huduma nyingine za afya.

(ii) Serikali kwa kushirikiana na wadau itaimarisha, kuendeleza na kuratibu tafiti za magonjwa ya kinywa.

(iii) Serikali ikishirikiana na wadau itaendelea kuwaelimisha wananchi juu ya afya ya kinywa.

### 5.4.6 Damu salama

**(a) Maelezo**

Mfumo wa damu salama unaotumika kwa sasa nchini ni ule wa kila hospitali kuwa na utaratibu wake wa kukusanya, kupima na kutumia damu. Aidha, mfumo huu unategemea zaidi ukusanyaji wa damu kutoka kwa ndugu wa wagonjwa kuliko kwa watoa damu wa kujitolea kwa hiari. Mfumo huu unasababisha kuwepo kwa uhaba wa damu na uwezekano wa maambukizo ya magonjwa yanayotokana na kuongezewa damu yenye matatizo au ugonjwa kama vile; UKIMWI, Kaswende, Homa ya Ini "*Hepatitis B na Hepatitis C*".

**(b) Madhumuni**

Kuimarisha mfumo wa kitaifa ambao unasimamia ukusanyaji, upimaji, utunzaji, usambazaji na matumizi ya damu salama nchini.

**(c) Tamko la sera**

(i) Serikali itaandaa na kusimamia sheria, kanuni, miongozo na taratibu za upatikanaji na matumizi ya damu salama.

(ii) Serikali itaboresha mazingira kwa wananchi, kuwawezesha kutoa damu kwa hiari.

(iii) Serikali kwa kushirikiana na wadau itaimarisha miundombinu ya upatikanaji, utunzaji na usambazaji wa damu salama.

(iv) Wananchi watahamasishwa, ili kuchangia huduma za upatikanaji wa damu salama.

### 5.4.7 Dawa za Kulevya na Afya ya Akili

**(a) Maelezo**

Afya ya akili ni sehemu muhimu ya huduma za afya ya jamii. Magonjwa na ulemavu wa akili vimekuwa vikiongezeka katika jamii kutokana na mabadiliko ya hali ya maisha na pia kuporomoka kwa mila na desturi nzuri ambazo ni muhimili na nyenzo za kinga dhidi ya magonjwa ya akili. Taratibu za jadi za kinga dhidi ya ulevi wa pombe wa kupindukia na matumizi ya dawa za kulevya zimelegalega katika jamii.

Huduma za afya ya akili nchini ni duni, kutokana na kutopewa umuhimu wake na upungufu wa wataalam wa magonjwa ya akili. Aidha, hakuna takwimu sahihi za hali halisi ya magonjwa ya akili na wenye ulemavu wa akili nchini. Vile vile, suala la unyanyapaa limeathiri upatikanaji wa huduma bora za afya ya akili.

**(b) Madhumuni**

Kupanua na kuimarisha wigo na ubora wa huduma za afya ya akili.

**(c) Tamko la sera**

(i) Serikali kwa kushirikiana na wadau itaimarisha mfumo wa huduma za kinga, tiba na utengamao wa matumizi ya dawa za kulevya na athari zake.

(ii) Serikali itapitia na kuboresha sheria, kanuni, miongozo na taratibu za kutoa huduma kwa wagonjwa wa akili, kwa kuzingatia utu na haki.

(iii) Serikali kwa kushirikiana na wadau wengine, itahakikisha kuwa huduma za afya ya akili zinawafikia wananchi wengi kulingana na mahitaji.

(iv) Serikali kwa kushirikiana na wadau, itaimarisha mfumo wa utoaji huduma na usimamizi wa huduma za afya ya akili nchini.

(v) Jamii itashirikishwa katika kuboresha utoaji wa huduma za afya ya akili.

(vi) Serikali kwa kushirikiana na wadau itaimarisha mfumo wa huduma za kinga dhidi ya dawa za kulevya, tiba na utengamao wa waathirika wa pombe na dawa za kulevya.

### 5.4.8 Ushirikishaji, Uchangiaji na Msamaha wa Huduma za Afya

#### 5.4.8.1 Ushiriki wa jamii katika upatikanaji huduma za afya

**(a) Maelezo**

Wananchi wamekuwa wakishiriki kwa hali na mali katika upatikanaji wa huduma za afya kwa kujenga, kukarabati na kutunza vituo vya huduma za afya. Aidha, wanashiriki katika uendeshaji kupitia bodi na kamati zao. Hata hivyo, ushiriki na ushirikishwaji wa wananchi katika upatikanaji na usimamizi wa huduma za afya bado uko chini.

**(b) Madhumuni**

Kuendeleza ushirikishaji wa jamii katika maamuzi ya upatikanaji, utoaji, uendeshaji na umiliki wa huduma za afya.

**(d) Tamko la sera**

(i) Serikali itakamilisha uundwaji wa Bodi na kamati za huduma za afya, katika ngazi mbalimbali na kuhakikisha kuwa zinatekeleza majukumu yao.

(ii) Serikali kwa kushirikiana na wadau wengine itahamasisha na kuweka mazingira mazuri, kwa wananchi kushiriki kikamilifu katika upatikanaji wa huduma za afya, ikiwa ni pamoja na; ujenzi, ukarabati, upangaji, uendeshaji na utumiaji wa vituo vya kutolea huduma.

#### 5.4.8.2 Uchangiaji wa gharama za huduma za afya

**(a) Maelezo**

Kutokana na athari za kuyumba kwa uchumi katika miaka ya 1980, gharama za utoaji wa huduma zimepanda. Aidha, ufinyu wa bajeti ya Serikali na ongezeko la watu vimesababisha bajeti ya Serikali na hasa ile ya sekta ya afya kuwa tegemezi kwa wahisani. Hii imefanya huduma hizi kutokuwa endelevu

na wananchi wenyewe kutoshiriki kuzimiliki kikamilifu. Kwa hali hii, katika mwaka 1993, Serikali iliamua kushirikisha wananchi katika kuchangia gharama za huduma za afya kupitia sera ya uchangiaji gharama. Pamoja na kuwepo kwa sera hii, bado uchangiaji hauridhishi na hivyo unatakiwa kuimarishwa.

**(b) Madhumuni**

Kupanua uwigo, kuimarisha na kuendeleza vyanzo vya mapato vya kuendeshea huduma za afya kwa nia ya kuboresha huduma na kupunguza utegemezi na kuimarisha ushiriki na umiliki wa huduma hizi kwa wananchi.

**(c) Tamko la sera**

(i) Serikali itaboresha na kuendelea kusimamia mikakati na miongozo ya uchangiaji wa gharama za huduma za afya pamoja na matumizi ya mapato yanayotokana na uchangiaji huo.

(ii) Serikali kwa kushirikiana na wadau itaendelea kubuni njia endelevu za kuchangia gharama za huduma za afya kwa manufaa ya wananchi wote kama vile Bima za Afya na Mifuko ya Afya ya Jamii.

**1.1.1.3 Msamaha wa uchangiaji gharama huduma za afya kwa makundi maalum**

**(a) Maelezo**

Serikali inatambua kuwepo kwa wananchi wasio na uwezo wa kuchangia gharama za huduma za afya, ikiwa ni pamoja na wale walio katika makundi maalum ya kijamii, mathalani; wazee walio na umri zaidi ya miaka 60 ambao hawana uwezo wa kipato, watoto wenye umri chini ya miaka mitano, watoto walio katika mazingira hatarishi**,** wanawake wajawazito na watu wasiojiweza kiuchumi. Pia, wenye magonjwa sugu kama; saratani, UKIMWI, kisukari, magonjwa ya moyo, pumu, *sickle cell,* kifua kikuu, ukoma na magonjwa ya akili.

**(b) Madhumuni**

Kuwezesha makundi maalum kupata huduma bora za afya sawa na wananchi wengine.

**(c) Tamko la sera**

(i) Serikali itaboresha, itaandaa na kusimamia sheria, kanuni na miongozo ya uchangiaji gharama za huduma za afya ikiwemo msamaha kwa makundi maalum.

(ii) Serikali itahakikisha kuna uwiano katika kutoa huduma za afya kwa makundi yote.

(iii) Serikali kwa kushirikiana na wadau itaandaa utaratibu mzuri wa namna ya kuyahudumia makundi maalum yanayostahili msamaha.

### 5.4.9 Ushirikishaji wa mashirika ya dini, asasi zisizo za kiserikali na sekta binafsi

**(a) Maelezo**

Serikali inatambua umuhimu wa mchango wa wadau toka sekta binafsi, mashirika ya dini na asasi zisizo za kiserikali katika utoaji wa huduma za afya. Hata hivyo, kuna udhaifu katika ushiriki na ushirikishwaji wa wadau wa sekta hiyo.

**(b) Madhumuni**

Kuboresha ushiriki wa mashirika ya dini na sekta binafsi ili kupanua uwigo wa kutoa huduma za afya na kuleta uwiano zaidi katika upatikanaji wake.

**(c) Tamko la sera**

(i) Serikali itaendelea kushirikisha mashirika ya dini na sekta binafsi katika utoaji wa huduma za afya kwa kutumia mikataba, makubaliano maalum na miongozo mbalimbali.

(ii) Serikali itaendelea kutambua na kushirikiana na mashirika ya dini na asasi mbalimbali zisizo za kiserikali katika kutoa huduma za afya na kulinda haki za makundi maalum.

(iii) Serikali itaweka na kusimamia viwango vya utoaji wa huduma za afya katika ngazi zote.

### 5.4.10 Huduma za afya binafsi

**(a) Maelezo**

Serikali inatambua mchango wa sekta binafsi, mashirika ya dini na asasi za hiari au zisizokuwa za kiserikali katika kupanua wigo wa utoaji wa huduma za afya nchini. Uanzishwaji wa huduma za afya binafsi umeongeza idadi ya vituo vya kutolea huduma za afya. Aidha, Serikali imeruhusu watumishi wa umma kutoa huduma za afya binafsi baada ya saa za kazi.

Mchango wa sekta binafsi umesaidia juhudi za Serikali katika kufikisha huduma za afya kwa wananchi, hasa pasipo na vituo vya umma. Hata hivyo, ongezeko la vituo binafsi limesababisha kuwepo kwa mahitaji makubwa ya wataalam wa afya kukidhi sekta za umma na binafsi. Hali hii imesababisha baadhi ya watumishi katika vituo vya umma kwenda kutoa huduma katika vituo vya afya binafsi.

Hata hivyo, imebainika kwamba baadhi ya watumishi wa umma hutumia muda wa saa za kazi kutoa huduma katika vituo vyao binafsi. Pamoja na nia njema ya Serikali, hali hii imesababisha malalamiko kwa watumiaji wa huduma katika vituo vya umma.

**(b) Madhumuni**

Kuweka mfumo madhubuti wa kusimamia huduma za afya zinazotolewa na watu binafsi, watumishi wa umma, mashirika ya dini na mashirika ya hiari au yasiyokuwa ya kiserikali.

**(c) Tamko la sera**

(i) Serikali itaimarisha utoaji wa huduma za afya za watu binafsi, watumishi wa umma, mashirika ya dini na mashirika ya hiari au yasiyokuwa ya kiserikali.

(ii) Serikali itatoa mwongozo wa watumishi wa umma kuhusu utoaji wa huduma za kitaalamu katika vituo vya kutolea huduma vya watu binafsi kulingana na sheria, kanuni na taratibu.

### 5.4.11 Tiba Asilia, Tiba Mbadala na Ukunga wa Jadi

**(a) Maelezo**

Tiba asilia inatumiwa na wananchi wengi. Takribani asilimia sitini ya wananchi huanza kutumia tiba asilia wanapopatwa na maradhi kabla ya kwenda vituo vya kutolea huduma za afya. Aidha, hivi karibuni tiba mbadala imepata umaarufu miongoni mwa wananchi kutokana na uimarikaji wake duniani.

Kadhalika, wagonjwa hutoka hospitalini na kwenda kutafuta tiba asilia au kutumia aina zote za tiba kwa pamoja. Vilele, takwimu zinaonyesha kwamba bado kuna wanawake wajawazito wanaojifungulia nyumbani kwa kusaidiwa na wakunga wa jadi. Pamoja na huduma hizi kutumiwa na wananchi wengi, uratibu wa uendeshaji wake unahitaji kuimarishwa.

**(b) Madhumuni**

Kuendeleza, kuratibu na kuboresha utoaji wa huduma za tiba asilia, mbadala na ukunga wa jadi.

**(c) Tamko la sera**

(i) Serikali itaandaa kanuni, miongozo na taratibu za usimamizi wa utoaji huduma za tiba asilia, tiba mbadala na ukunga wa jadi.

(ii) Watoa huduma za tiba asilia, tiba mbadala na ukunga wa jadi watashirikishwa kuboresha na kusimamia utoaji wa huduma hizo.

(iii) Wadau watashirikishwa katika kuweka mfumo madhubuti wa kulinda mazingira na mimea inayotumika katika tiba asilia na tiba mbadala.

(iv) Serikali kwa kushirikiana na wadau itaimarisha, kuendeleza na kuratibu tafiti za tiba asilia, tiba mbadala na ukunga wa jadi.

## 5.5 Huduma za Utengemao

**(a) Maelezo**

Inajumuisha juhudi mbalimbali zinazofanywa ili kumwezesha mtu mwenye ulemavu kuona kuwa ulemavu sio kikwazo cha maendeleo yake na kuwa anaweza kuvitumia viungo alivyonavyo kujiendeleza, katika nyanja mbalimbali kama watu wengine. Huduma hizi, ziko katika nyanja za kijamii na kitabibu.

Juhudi hizi ni pamoja na kutoa ushauri nasaha kwa mhusika ili aikubali hali yake na kumshauri kuhusu kazi anazoweza kuzifanya zikamnufaisha yeye na taifa kwa ujumla.

Aidha, kuishauri familia yake na jamii inayomzunguka kumhamasisha kujiendeleza ili aweze kujitegemea. Juhudi zinaendelea kumsaidia mwathirika kupewa mazoezi ya viungo kuimarisha viungo vilivyoko, mazoezi ya kiakili ya kuamsha upya hali ya ubongo na kuwekewa viungo bandia pale mhusika anapopoteza kiungo kama mkono au mguu.

**(b) Madhumuni**

Kuwawezesha watu wenye ulemavu kupatiwa huduma na nyenzo zitakazomuwezesha angalau kupunguza athari za hali ya ulemavu.

**(c) Tamko la sera**

(i) Serikali kwa kushirikiana na wadau, itajenga mfumo utakaowezesha watu wenye ulemavu kutambuliwa mapema na kupatiwa tiba katika ngazi zote za uotaji huduma.

(iii) Serikali kwa kushirikiana na wadau itaweka mfumo utakaowezesha watu wenye ulemavu kupatiwa vifaa vya kujimudu kama vile; miguu ya bandia, magongo, viatu maalum, fimbo nyeupe, kofia na miwani.

(iv) Serikali kwa kushirikiana na wadau itaendelea kuweka mazingira mazuri ya kutoa huduma za utengemao katika ngazi zote.

## 5.6 Maendeleo ya Watumishi na Vyuo vya Mafunzo vya Sekta ya Afya

### 5.6.1 Maendeleo ya watumishi

**(a) Maelezo**

Ili kuendelea kutoa huduma za afya zilizo bora, watumishi katika sekta ya afya wanahitaji kuwa na mafunzo endelevu kazini. Kumekuwepo na juhudi za Serikali za kuwaendeleza watumishi katika sekta hii ambazo zimewahusisha watumishi katika ngazi zote. Mafunzo ambayo yamekuwa yanatolewa yamekuwa yakilenga mambo mapya ambayo yamekuwa yakijitokeza, kama magonjwa na maendeleo ya teknolojia katika sekta ya afya. Mafunzo haya, yamekuwa yanafanyika katika sehemu za kazi, nje ya vituo vya kazi kwa mafunzo ya muda

mfupi na mrefu.

Katika kuhahikikisha kwamba mafunzo yanatolewa katika maeneo yenye kipaumbele, Wizara imetengeneza mpango wa kuwaendeleza watumishi wa afya nchini. Pamoja na juhudi hizi, wapo baadhi ya watumishi ambao baada ya mafunzo wamekuwa wakipangwa sehemu tofauti na elimu waliyosomea.

Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa kushirikiana na Mabaraza ya Ithibati pamoja na Mabaraza husika ya Taaluma wanahakikisha kwamba mafunzo yatolewayo katika sekta ya afya yana ubora kwa kuandaa mitaala inayokidhi mahitaji ya afya kitaifa na usimamizi wake.

**(b) Madhumuni**

Kuwa na watumishi wenye ujuzi unaohitajika ili waweze kutoa huduma sahihi, kuongoza na kuendesha utoaji wa huduma bora kulingana na mahitaji ya wakati wote.

**(c) Tamko la sera**

(i) Serikali kwa kushirikiana na wadau itaimarisha mpango wa kuwaendeleza watumishi na wataalam wote wa sekta ya afya, ili kufikia viwango vya ubingwa na maalum.

(ii) Watumishi na wataalamu wa afya waliohitimu mafunzo ya kujiendeleza watapangwa sehemu za kazi kulingana na mahitaji na ujuzi walioupata.

(iii) Serikali itaendelea kusimamia mitaala na kutoa miongozo ya mafunzo inayozingatia viwango bora vya ufundishaji katika vyuo vya umma na vile vya watu binafsi, mashirika ya dini, mashirika yasio ya kiserikali, ili kukidhi viwango vya kitaifa na kimataifa.

### 5.6.2 Vyuo vya mafunzo ya afya.

**(a) Maelezo**

Serikali na wadau wamefanya juhudi kubwa katika kuanzisha vyuo mbalimbali vya kutoa mafunzo ya afya. Hata hivyo, idadi ya vyuo, na idadi ya wahitimu pamoja na ubora wa mafunzo yanayotolewa hayatoshelezi matarajio ya jamii, ongezeko la watu na  mabadiliko ya teknolojia. Aidha, kutokana na gharama kubwa za kuendesha vyuo vya mafunzo, Serikali ilianzisha utaratibu wa

uchangiaji wa gharama za mafunzo ya afya.

Pamoja na nia nzuri ya Serikali, hali hii imesababisha baadhi ya wanafunzi kushindwa kumudu gharama za masomo. Wizara kwa kushirikiana na mabaraza ya kitaaluma pamoja na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi, wanaendelea kusimamia na kuhakikisha ubora wa mafunzo ya afya yanayotolewa. Hata hivyo, uzalishaji wa wataalamu mbalimbali wa afya umekuwa wa kiwango cha chini ukilinganisha na mahitaji.

**(b) Madhumuni**

Kupata wataalam wa kutosha, wenye ujuzi wa kutoa huduma bora katika ngazi zote, ikiwa ni pamoja na wataalam wa usimamizi na uendeshaji wa sekta ya afya.

**(c) Tamko la sera**

(i) Serikali kwa kushirikiana na wadau, itaongeza na kuratibu vyuo vya mafunzo ya afya na wahitimu kulingana na mahitaji ya taifa.

(ii) Serikali kupitia asasi za kusimamia ithibati na mabaraza ya kitaaluma itasimamia viwango vya ubora wa mafunzo katika vyuo vya afya.

(iii) Serikali itaendelea kushirikiana na mashirika ya dini na sekta binafsi katika kuongeza nafasi za mafunzo ya huduma za afya.

(iv) Serikali na wadau wengine itahakikisha kwamba nafasi za mafunzo ya afya zinatolewa kwa kuzingatia usawa wa jinsia.

(v) Serikali itaimarisha utaratibu wa kuchangia gharama za mafunzo na kuanzisha utaratibu wa mikopo kwa wanafunzi katika vyuo vya afya kwa kuzingatia sheria na miongozo iliyopo, ili kuongeza idadi ya wahitimu kwenye vyuo hivyo.

## 5.7 Raslimali

### 5.7.1 Watu

**(a) Maelezo**

Raslimali watu katika sekta ya afya ni moja kati ya raslimali muhimu katika kutoa huduma za afya. Serikali imefanya jitihada katika kuboresha raslimali hii kwa njia mbalimbali, ikiwa ni pamoja na kuongeza idadi ya wataalamu,

kuboresha ujuzi katika nyanja mbali mbali, kuongeza mishahara na masilahi mengine kwa wafanya kazi.

Pamoja na jitihada hizi, kuna vikwazo kadhaa vinavyoathiri huduma za afya zitolewazo kwa wananchi, ikiwa ni pamoja na upungufu wa wataalamu uliokithiri, hususan; maeneo ya vijijini na sehemu za pembezoni. Hii ni pamoja na uwiano usiokidhi wa ujuzi na idadi ya wataalamu kufuatana na ikama iliyowekwa.

Kutokana na ongezeko la maradhi pamoja na mabadiliko ya teknolojia ya matibabu, inalazimu watumishi wa sekta ya afya wawe na ujuzi pamoja na mbinu mbalimbali za kukabiliana nayo.

**(b) Madhumuni**

Kuwa na raslimali watu ya kutosha, iliyohamasika na yenye ujuzi wa kutoa huduma bora za afya.

**(c) Tamko la sera**

(i) Kuwepo kwa watumishi wa kutosha na wenye ujuzi katika taaluma mbalimbali, katika ngazi zote za kutolea huduma kulingana na vigezo vilivyokubalika.

(ii) Uboreshaji wa mazingira ya kazi, ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa vitendea kazi vya kutosha kwa watumishi wa afya.

(iii) Kuhamasisha taasisi, mashirika na wadau wengine kuanzisha na kuongeza vyuo vya taaluma ya huduma za afya.

(iv) Kuweka vivutio katika sehemu zenye mazingira magumu na hatarishi, ili kuwavutia wataalam kwenda kufanya kazi katika sehemu hizo.

(v) Uimarishaji wa vituo vya kanda, ili viweze kuzalisha raslimali watu kwa ajili ya sekta ya afya na kusimamia uboreshaji wa huduma za afya katika sehemu zao.

### 5.7.2 Fedha

**(a) Maelezo**

Serikali imekuwa ikiongeza bajeti ya sekta ya afya kila mwaka, ili kukidhi mahitaji muhimu ya afya kwa wananchi wake. Hata hivyo, nyongeza hiyo imekuwa haikidhi mahitaji halisi ya kutolea huduma, kwa sababu ya kuongezeka

kwa gharama za kukinga na kutibu magonjwa mbalimbali zikiwemo, usugu wa vimelea vya magonjwa, mabadiliko ya teknolojia na mfumuko wa bei.

Vilevile, kuna uhaba mkubwa wa vitendea kazi na vile vilivyopo, vingi ni chakavu, havina matengenezo na vimepitwa na teknolojia ya kisasa.

**(b) Madhumuni**

Kuendelea kuongeza bajeti ya sekta ya afya, ili kuboresha upatikanaji wa huduma.

**(c) Tamko la sera**

(i) Serikali itaendelea kuongeza bajeti ya sekta ya afya, mwaka hadi mwaka, ili kufikia Azimio la Abuja la asilimia 15 ya bajeti ya Serikali, kwa lengo la kukidhi mahitaji muhimu ya kisekta.

(ii) Serikali itatekeleza mikataba mbalimbali ya kimataifa ambayo imeridhia, katika kufikia malengo mbalimbali katika sekta ya afya.

(iii) Serikali itaimarisha na kupanua vyanzo vya uchangiaji gharama za huduma za afya.

(iv) Serikali kwa kushirikiana na wadau itaimarisha na kubuni vyanzo mbalimbali vya uchangiaji gharama za huduma za afya, ili kuongeza raslimali fedha ambazo ni endelevu, ili kuboresha huduma za afya nchini.

(v) Serikali itaimarisha mfumo endelevu wa matengenezo kinga, na matengenezo ya vifaa.

## 5.8 Mipango ya Afya

### 5.8.1 Mipango na Uratibu

**(a) Maelezo**

Huduma za afya zinatolewa na wadau mbalimbali, ikiwa ni pamoja na watu binafsi, mashirika ya dini na ya hiari, asasi za kijamii na taasisi za Serikali. Kutokana na hali hii, Serikali inawajibika kuratibu kwa karibu utoaji wa huduma kulingana na viwango vilivyowekwa, mahitaji halisi na matumizi bora ya raslimali.

**(b) Madhumuni**

Kuwa na mfumo madhubuti, mipango na usimamizi shirikishi na endelevu katika sekta ya afya pamoja na watoa huduma, ili kuwa na uwazi, matumizi bora ya raslimali na kuhakiki viwango vya huduma zinazotolewa.

**(c) Tamko la sera**

(i) Serikali itaendelea kuandaa na kuboresha sheria, kanuni, miongozo na taratibu za kufuatwa na wadau wote katika utoaji huduma za afya.

(ii) Serikali kwa kushirikiana na wadau itasimamia na kuratibu huduma za afya zitolewazo na wadau katika ngazi mbalimbali.

### 5.8.2 Ubora na viwango vya huduma

**(a) Maelezo**

Serikali imeweka viwango vya ubora katika utoaji wa huduma za afya. Hata hivyo, huduma za afya hapa nchini hazijafikia viwango vinavyotakiwa. Aidha, kuna upungufu wa wataalam katika ngazi zote, uchakavu wa majengo, upungufu wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendea kazi. Vilevile, mazingira ya kufanyia kazi bado ni duni. Hali hii imesababisha malalamiko kutoka kwa wananchi.

**(b) Madhumuni**

Kuinua na kuboresha huduma za afya katika maeneo yote ya sekta ya afya, ili kufikia viwango vinavyokubalika.

**(c) Tamko la sera**

(i) Serikali itaweka na kuimarisha viwango vya ubora wa huduma za afya.

(ii) Serikali itaweka mfumo wa kusimamia na kukagua ubora wa huduma za afya.

(iii) Serikali itaweka na kusimamia viwango vya watumishi wenye ujuzi unaotakiwa wa kutolea huduma sehemu mbalimbali.

### 5.8.3 Ufuatiliaji na tathmini

**(a) Maelezo**

Mojawapo ya majukumu ya Wizara ni kufanya ufuatiliaji na tathmini, ili kuhakikisha kuwa huduma zitolewazo katika vituo vyote vya kutolea huduma za afya zinakidhi viwango vilivyowekwa. Pamoja na juhudi zilizofanyika, bado ubora wa huduma uko chini ya viwango na hakuna mfumo rejea ulio rahisi, shirikishi na endelevu.

**(b) Madhumuni**

Kuwa na mfumo wa ufuatiliaji, tathmini na rejea wa kutolea huduma za afya, katika ngazi zote ulio rahisi, shirikishi na endelevu.

**(c) Tamko la sera**

(i) Serikali itaimarisha ufuatiliaji wa ubora wa huduma za afya kulingana na vigezo vya upimaji, matumizi ya raslimali, utendaji kazi na rejea.

(ii) Serikali itaendelea kuimarisha mifumo ya ukusanyaji na matumizi ya taarifa katika ngazi zote za kutolea huduma.

(iii) Serikali itaweka viwango vya ubora wa huduma kitaifa na miongozo inayohusu vituo vya kutolea huduma, majengo na vifaa, uongozi na ikama ya watumishi.

(iv) Serikali itashirikisha sekta binafsi katika kufuatilia na kutathmini utoaji wa huduma zilizo bora na zenye uwiano.

### 5.8.4 Ukusanyaji na utumiaji wa takwimu

**(a) Maelezo**

Takwimu ni muhimu katika kutoa vigezo mbalimbali, ambavyo hutumika kutathmini huduma za afya zitolewazo na kupima matokeo ya huduma hizo. Aidha, takwimu ni muhimu katika kuandaa mipango mbalimbali, kuboresha sera, na kusaidia katika kutoa maamuzi mbalimbali. Utaratibu uliopo wa kukusanya takwimu za afya unategemea mifumo mbalimbali iliyopo katika jamii. Hata hivyo, kuna udhaifu katika kuratibu mifumo hiyo, kuhakiki ubora wa takwimu, kuchambua, kutafsiri na kutumia takwimu.

**(b) Madhumuni**

Kuimarisha uboreshaji na usahihi wa mifumo mbalimbali ya ukusanyaji takwimu na kuweka utaratibu mzuri wa kuratibu mifumo hiyo.

**(b) Tamko la Sera**

(i) Serikali itaratibu, itasimamia na itaimarisha mifumo ya ukusanyaji wa takwimu za afya sahihi katika ngazi zote kwa kushirikisha wadau.

(ii) Serikali kwa kushirikisha wadau mbalimbali, itaimarisha mifumo ya takwimu, ikiwa ni pamoja na; kutoa mafunzo, kuandaa miongozo ya kukusanya, kutunza, kuchambua na (kutumia) matumizi sahihi ya takwimu hizo kwa manufaa ya wananchi.

(iii) Serikali itakuwa mmiliki mkuu wa takwimu zitokanazo na mifumo iliyo chini yake, pamoja na zile zinazopatikana kwa kushirikiana na wadau mbalimbali katika kupata takwimu.

(iv) Serikali itatoa mjibuko/mrejesho wa matokeo ya takwimu kwa wakusanyaji na wadau wengine.

### 5.8.5 Utafiti

**(a) Maelezo**

Utafiti ni udadisi wa kisayansi unaolenga kugundua na kubainisha suala au tatizo fulani. Serikali inatambua umuhimu wa kufanya utafiti, na kutumia matokeo ya utafiti katika kuboresha utoaji wa huduma za afya . Tafiti nyingi za kuboresha huduma za afya zimefanyika na baadhi zimeweza kubainisha ukubwa wa maradhi kama; Malaria, UKIMWI, Kifua Kikuu na hata kubainisha usugu wa vimelea katika baadhi ya dawa zinazotumika katika matibabu. Hata hivyo, baadhi ya tafiti zinaendelea kufanyika bila kuzingatia vipaumbele na changamoto za afya. Pia, tafiti hizo, hazikidhi mahitaji ya sekta ya afya katika kuboresha huduma.

**(b) Madhumuni**

Kuimarisha mfumo wa tafiti zitakazosaidia kuboresha utoaji huduma za afya, kwa kutumia matokeo ya tafiti hizo.

(c) **Tamko la sera**

(i) Serikali itaimarisha mfumo wa utafiti na kutumia matokeo ya utafiti katika kupanga na kutekeleza mikakati na mipango ya afya.

(ii) Serikali itaendelea kutenga fedha za kufanyia tafiti muhimu za afya kila inapowezekana.

(iii) Serikali itasimamia na kuratibu tafiti zote za afya zinazofanyika nchini.

(iv) Serikali itaendelea kutunga na kuimarisha sheria, taratibu, kanuni na miongozo inayosimamia na kulinda matumizi ya bioanuai iliyopo nchini.

(v) Serikali itatunga na kuimarisha sheria, taratibu, kanuni na miongozo inayosimamia hatimiliki ya matokeo ya tafiti.

## 5.9 Huduma Nyingine

### 5.9.1 Udhibiti wa kemikali na uchambuzi wa chembe hai na viini tete

**(a) Maelezo**

Kutokana na kukua kwa uwezo wa tafiti na teknolojia ya tiba, matumizi ya chembe hai na viini tete yamekuwa yakiongezeka duniani. Katika nchi zilizoendelea, teknolojia ya chembe hai na viini tete kwa sasa inatumika kwa matumizi mengi, ikiwa ni pamoja na; matibabu ya magonjwa ya urithi na kusaidia wanawake wagumba kupata mimba. Aidha, kumekuwa na majadiliano ya kutumia chembe hai na viini tete katika kuumba binadamu jambo ambalo kimataifa halijakubaliwa.

**(b) Madhumuni**

Kuweka mfumo wa matumizi sahihi na salama ya teknolojia ya chembe hai na viini tete, ili kulinda afya ya wananchi, viumbe hai vingine, mazingira na usalama wa taifa letu.

(c) **Tamko la sera**

(i) Serikali itatunga sheria na kuandaa kanuni, miongozo na taratibu za matumizi sahihi ya chembe hai na viini tete na kusimamia utekelezaji wake.

### 5.9.2 Usimamizi na udhibiti wa ubora wa chakula, dawa, vipodozi, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi

**(a) Maelezo**

Serikali ina vyombo kadhaa vya kusimamia viwango na ubora wa bidhaa zinazozalishwa nchini na zinazoingizwa kutoka nje ya nchi. Kuongezeka kwa biashara huria na utandawazi, kumechochea kuwepo kwa bidhaa nyingi za chakula, dawa, vipodozi, kemikali, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi hapa nchini. Hali hii ni changamoto katika kusimamia na kudhibiti viwango vya ubora, usalama na ufanisi wa bidhaa hizo.

**(b) Madhumuni**

Kuhakikisha kuwa bidhaa za chakula, dawa, vipodozi, kemikali, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi vinavyotumika nchini ni salama na vyenye viwango vya ubora unaokubalika, ili kulinda afya ya jamii.

**(c) Tamko la sera**

(i) Serikali itaandaa na kuboresha sheria, kanuni, miongozo, taratibu na mifumo ya kusimamia udhibiti wa bidhaa za chakula, dawa, vipodozi, kemikali, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi.

(ii) Serikali kwa kushirikiana na wadau itaimarisha utaratibu wa kuboresha udhibiti na uendeshaji biashara za chakula, dawa, vipodozi, kemikali, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi.

(iii) Serikali kwa kushirikiana na wadau itaimarisha ufuatiliaji na utafiti wa madhara yatokanayo na matumizi ya chakula, dawa, vipodozi, kemikali, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi.

(iv) Mfumo na miundombinu ya kudhibiti bidhaa za chakula, dawa, vipodozi, kemikali, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi vitaimarishwa.

(v) Miongozo ya matumizi sahihi ya chakula, dawa, vipodozi, kemikali, vifaa, vifaa tiba, vifaa vya utengamao na vitendanishi itaandaliwa.

(vi) Watengenezaji wa bidhaa za chakula, dawa, vipodozi, kemikali, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi vyenye viwango vinavyokubalika watashirikishwa katika kuboresha mazingira ya uzalishaji.

### 5.9. 3 Udhibiti wa kemikali, uchunguzi wa sampuli mbalimbali na matumizi ya vinasaba

**(a) Maelezo**

Mfumo madhubuti wa uchunguzi na ufuatiliaji wa magonjwa ni muhimu katika utoaji na uboreshaji wa huduma za afya na tiba. Aidha, uchunguzi wa vyanzo vya makosa ya jinai na vifo ni muhimu katika upatikanaji wa haki za kisheria. Vilevile, uchunguzi wa vinasaba ni muhimu katika kubaini maradhi ya urithi na pia, katika upatikanaji wa haki kisheria.

Aidha, kumekuwa na maendeleo makubwa duniani ya matumizi ya vinasaba katika utafiti, matibabu, uchunguzi na uzalishaji wa mimea, vyakula na wanyama.

Mfumo wa uchunguzi wa magonjwa hapa nchini hauendani na mabadiliko katika maendeleo ya teknolojia ya uchunguzi na matumizi ya vinasaba. Matumizi hafifu ya huduma za uchunguzi yamechangia katika kutolewa kwa tiba bila ya kuwa na vipimo sahihi.

**(b) Madhumuni**

Kuweka mfumo madhubuti wa uchunguzi wa magonjwa na vinasaba, kuwezesha tiba sahihi na upatikanaji wa haki za kisheria.

**(c) Tamko la sera**

(i) Serikali itaandaa sheria, kanuni, miongozo na taratibu za kusimamia mfumo wa uchunguzi wa magonjwa na vinasaba.

(ii) Serikali kwa kushirikiana na wadau itaimarisha upatikanaji na matumizi ya vifaa vya uchunguzi vya kisasa.

(iii) Serikali itashirikiana na wadau wa ndani na nje ya nchi, katika kutekeleza mikataba ya kimataifa ambayo nchi imeridhia kuhusu matumizi sahihi ya kemikali.

## 5.10 Wakala na Taasisi zilizopo chini ya Wizara

### 5.10.1 Bohari ya Dawa ya Serikali

**(a) Maelezo**

Dawa na vifaa tiba ni bidhaa muhimu katika kutoa huduma za afya zilizo bora. Bidhaa hizi zinahitaji utaalamu na umakini mkubwa wakati wa kuagiza, kutunza na kusambaza. Jukumu hilo lilikabidhiwa Bohari Kuu ya Dawa. Hata hivyo, uendeshaji wake haukukidhi matarajio na mahitaji yaliyokusudiwa. Hivyo, Serikali iliunda Bohari ya Dawa ya Serikali kwa Sheria namba 13 ya mwaka 1993.

**(b) Madhumuni**

Kuunda na kusimamia mfumo unaokidhi haja na wenye unafuu wa ununuzi, uhifadhi na usambazaji wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi vya maabara vinavyohitajika nchini kwa wakati wote.

**(c) Tamko la Sera**

(i) Uagizaji, utunzaji na usambazaji wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi utashughulikiwa na Bohari ya Dawa ya Serikali kulingana na Sheria namba 13 ya mwaka 1993.

(ii) Bohari ya Dawa ya Serikali itaendelea kufungua Bohari za Kanda na Mikoa ili kusogeza huduma karibu na wananchi.

### 5.10.2 Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu

**(a) Maelezo**

Utafiti wa magonjwa ya binadamu ni moja ya mkakati muhimu unaochangia uboreshaji wa huduma za uchunguzi, kinga na tiba. Taasisi mbalimbali zimekuwa zikifanya tafiti za magonjwa ya binadamu bila uratibu na ufuatiliaji wa chombo cha Serikali. Hali hii imesababisha wakati mwingi matokeo ya tafiti hizo kutotumika ipasavyo na hata kutowafikia walengwa. Kwa kutambua upungufu huu, Serikali ilianzisha Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu, kwa Sheria namba 23 ya mwaka 1979, iliyofanyiwa mapitio mwaka 2002.

**(b) Madhumuni**

Kuendeleza na kuimarisha tafiti za magonjwa ya binadamu, ili kutumia matokeo ya tafiti hizo kuboresha huduma za kinga na tiba.

**(c) Tamko la Sera:**

(i) Kusimamia, kuratibu na kuendesha tafiti za magonjwa ya binadamu na kutumia matokeo ya tafiti hizo kuboresha huduma za afya.

### 5.10.3 Wakala wa Maabara ya Mkemia wa Serikali

**(a) Maelezo**

Serikali ina jukumu la kutoa na kusimamia huduma za uchunguzi wa sampuli za bidhaa za viwandani na mashambani, kusimamia udhibiti wa kemikali, ili kulinda afya za wananchi, mazingira na ubora wa bidhaa katika soko la ndani kwa nia ya kukuza biashara na pato la Taifa. Pia, Serikali ina jukumu la kutoa na kusimamia huduma za uchunguzi wa sampuli za kijinai na toksikolojia ili kutoa haki na utengamano katika jamii. Vipimo vya maabara na udhibiti wa kemikali vinatakiwa kuwa bora na vyenye kuaminika ndani na nje ya nchi. Ili kutekeleza majukumu haya, Serikali ilianzisha Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali mwaka 1999, kwa mujibu wa Sheria ya kuanzishwa Wakala za Serikali Na. 30 ya mwaka 1997.

**(b) Madhumuni**

Kuimarisha huduma za maabara katika uchunguzi wa ubora na usalama wa vyakula, dawa, kemikali, maji, maji taka, sampuli za kijinai, toksikolojia, vinasaba, udhibiti wa kemikali na tafiti, ili kulinda afya za wananchi, mazingira na kusaidia vyombo vya dola kufikia maamuzi sahihi na kutoa haki.

**(c) Tamko la sera**

(i) Uchunguzi wa sampuli na udhibiti wa kemikali utafanywa na Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali kulingana na sheria iliyounda Wakala hiyo.

(ii) Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali itazingatia sheria, miongozo na kanuni zinazoelekeza na kusimamia utoaji wa matokeo ya uchunguzi wa sampuli za kijinai na toksikolojia kwa ubora na wakati, ili kutoa haki kwa watuhumiwa wa makosa ya jinai ,wadai na wadaiwa kwa nia ya kuleta utengamano katika jamii.

### 5.10.4 Mamlaka ya Chakula na Dawa

**(a) Maelezo**

Kuongezeka kwa biashara huria na utandawazi kumechochea kuwepo kwa bidhaa nyingi za vyakula, dawa, vipodozi, vifaa tiba na vitendanishi nchini. Hali hii ni changamoto kwa Serikali katika kulinda afya za watumiaji dhidi ya madhara yatokanayo na matumizi ya bidhaa hizo. Aidha, uwepo wa vyakula, dawa, vipodozi na vifaa tiba bandia na visivyofikia viwango vilivyowekwa vya ubora na usalama ni changamoto nyingine inayohitaji mfumo thabiti wa udhibiti. Kwa kutambua hali hiyo, Serikali ilianzisha Mamlaka ya Chakula na Dawa kwa Sheria namba 1 ya mwaka 2003.

**(b) Madhumuni**

Kuwa na mfumo madhubuti wa kusimamia na kudhibiti vyakula, dawa, vipodozi, vifaa tiba na vitendanishi vinavyotengenezwa hapa nchini na vile vinavyoagizwa kutoka nje ili kulinda afya ya wananchi.

**(c) Tamko la Sera**

(i) Udhibiti wa ubora wa bidhaa za chakula, dawa, vipodozi,vifaa tiba na vitendanishi utasimamiwa na Mamlaka ya Chakula na Dawa kulingana na Sheria namba 1 ya mwaka 2003.

(ii) Mamlaka kwa kushirikiana na wadau, itaendelea kufuatilia na kutafiti madhara yatokanayo na matumizi ya vyakula, dawa, vipodozi, vifaa tiba na vitendanishi.

### 1.1.1 Taasisi ya Chakula na Lishe

**(a) Maelezo**

Utapiamlo nchini unaendelea kuwa tatizo kubwa kwa wananchi wote kwa viwango tofauti. Hata hivyo, makundi yanayoathirika zaidi na tatizo hili ni; watoto wadogo wenye umri chini ya miaka mitano, wanawake wajawazito na wale wanaonyonyesha. Athari za utapiamlo kwa watoto wadogo ni ukuaji duni kimwili na kiakili. Aidha, takwimu zilizopo zinaonyesha kuwa utapiamlo unachangia zaidi ya asilimia 50 ya vifo vya watoto wenye umri chini ya miaka mitano. Utapiamlo unasababisha wanawake wajawazito kuzaa watoto wenye uzito pungufu na pia, unaweza kusababisha vifo miongoni mwao.

Kwa kutambua tatizo hili, Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali za

kukabiliana nalo. Hatua hizo zimejumuisha kuanzishwa kwa Taasisi ya Chakula na Lishe kwa Sheria namba 24 ya mwaka 1973 na kurekebishwa na Sheria namba 3 ya mwaka 1995.

**(b) Madhumuni**

Kuboresha huduma za lishe zitolewazo na sekta ya umma, sekta binafsi na asasi za kiraia nchini, hasa kwa makundi yanayoathirika zaidi kilishe.

**(c) Tamko la Sera**

(i) Taasisi itaratibu na kusimamia utekelezaji wa mikakati, mipango na miradi mbalimbali inayolenga kuboresha lishe.

(ii) Taasisi kwa kushirikiana na wadau wengine itaendelea kuelimisha jamii na kujenga uwezo wa watendaji na watoa huduma za lishe ngazi zote, ili kutoa huduma bora za lishe.

(iii) Taasisi kwa kushirikiana na wadau wengine itaratibu utarayarishaji wa miongozo, viwango, kanuni na taratibu zitakazolinda ubora wa huduma za lishe zitolewazo nchini.

(iv) Taasisi itahamasisha wadau mbalimbali kuwekeza katika lishe.

(v) Taasisi itaweka mazingira mazuri ya kuhamasisha uendeshaji wa tafiti mbalimbali katika nyanja ya lishe na kulishauri Taifa juu ya lishe bora.

### 5.10.5 Taasisi ya Saratani ya Ocean Road

**(a) Maelezo**

Ugonjwa wa saratani umekuwepo nchini kwa muda mrefu. Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali za kukabiliana na ugonjwa huo. Miongoni mwa hatua hizo ni kuanzishwa kwa Taasisi ya Saratani ya Ocean Road kwa Sheria namba 2 ya mwaka 1996. Taasisi hii ni maalumu kwa huduma za uchunguzi, kinga na tiba kwa ugonjwa wa saratani. Aidha, Taasisi hii ndio kituo pekee cha kutibu saratani za aina mbalimbali. Ili kupunguza kero na usumbufu wa wagonjwa wanaotoka sehemu mbalimbali nchini kufuata uchunguzi na matibabu, Taasisi itaanzisha vituo vya tiba katika hospitali za mikoa.

**(b) Madhumuni**

Kutoa huduma za kinga, tiba kwa ugonjwa wa saratani na kufanya tafiti

zinazohusu ugonjwa wa saratani, ili kudhibiti kuenea kwa ugonjwa na kutoa tiba sahihi na bora kwa wagonjwa.

**(c) Tamko la Sera**

(i) Taasisi kwa kushirikiana na wadau itaendelea kutoa huduma za ubingwa maalum za uchunguzi, kinga na matibabu kwa wagonjwa wa Saratani.

(ii) Taasisi kwa kushirikiana na wadau mbalimbali itaendelea kufanya utafiti katika nyanja mbalimbali za saratani.

(iii) Taasisi itaendelea kutoa elimu kwa jamii, ili iweze kuzuia na kujikinga na saratani.

(iv) Taasisi itashirikiana na hospitali za mikoa kutoa huduma za nje ya kituo (outreach services), ili kuwafikia wananchi wengi zaidi nchini.

### 5.10.6 Taasisi ya Mifupa MOI

**(a) Maelezo**

Taasisi ya Mifupa – MOI iliyoanzishwa kwa Sheria Na. 7 ya mwaka 1996, ni mojawapo ya hospitali maalumu zilizo chini ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii. Taasisi inatoa huduma kwa ngazi ya rufaa katika upasuaji wa mifupa, upasuaji wa ubongo na mishipa ya fahamu na majeruhi.

Vilevile, Taasisi kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Sayansi za Afya cha Muhimbili (MUHAS) kinatoa mafunzo kwa ngazi ya shahada ya kwanza na uzamili katika fani hizo. Taasisi pia, inafanya utafiti katika fani ya upasuaji wa mifupa, ubongo na mishipa ya fahamu na majeruhi. Pamoja na kuanzishwa kwa huduma hizi hapa nchini, bado hazijawafikia wananchi wengi wanaozihitaji. Aidha, kutokana na upungufu wa wataalamu na vifaa vya kitaalamu, inalazimu Serikali kupeleka nje ya nchi baadhi ya wagonjwa kwa uchunguzi na matibabu ya ubingwa maalum.

**(b) Madhumuni**

Kuimarisha mfumo wa utoaji huduma kwa ngazi ya rufaa katika upasuaji wa mifupa, ubongo na mishipa ya fahamu na majeruhi, na upatikanaji wa wataalamu wa utafiti katika fani hizo, ili kutoa huduma za ngazi zote pamoja na za ubingwa maalum hapa nchini.

**(c) Tamko la Sera**

(i) Taasisi itasimamia utoaji huduma kwa ngazi ya rufaa na za ubingwa maalum katika fani ya upasuaji wa mifupa, ubongo na mishipa ya fahamu na majeruhi kwa kuzingatia Sheria namba 7 ya mwaka 1996.

(ii) Taasisi kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Sayansi za Afya cha Muhimbili, itafundisha wataalamu wa afya ngazi ya shahada ya kwanza, uzamili na uzamivu katika fani za upasuaji wa mifupa, ubongo na mishipa ya fahamu na majeruhi.

(iii) Taasisi itafanya utafiti katika fani ya upasuaji wa mifupa, ubongo na mishipa ya fahamu, ili kuboresha utoaji huduma katika fani hizo.

(iv) Taasisi itaendelea kuimarisha huduma za ngazi zote mpaka huduma za ubingwa maalum katika fani ya upasuaji wa mifupa, ubongo na mishipa ya fahamu na majeruhi, ili kuipunguzia Serikali mzigo wa kupeleka wagonjwa nje ya nchi kwa matibabu katika fani hizo.

### 5.10.7 Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya

**(a) Maelezo**

Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ulianzishwa kwa Sheria namba 8 ya mwaka 1999. Mfuko huu ni wa uchangiaji (Mwajiri na Mwajiriwa) kwa Watumishi katika sekta ya Umma. Mfuko ulianza kutoa huduma mwaka 2001, na unakua mwaka hadi mwaka, sambamba na uboreshaji wa mafao kwa Wanufaika pamoja na uboreshwaji wa huduma katika vituo vya kutolea huduma.

Sheria iliyoanzisha Mfuko huu, hairuhusu uanachama kutoka Sekta nje ya Utumishi wa Umma. Hata hivyo, makundi mbalimbali yaliyo nje ya Utumishi wa Umma, yamekuwa yakiomba kujiunga na Mfuko, na Serikali inalifanyia kazi suala hili ili hatimaye wananchi wote wajiunge na Mfuko huu.

**(b) Madhumuni**

Kuwa na mfumo madhubuti na endelevu wa uchangiaji wa huduma za Afya kwa watumishi wa Umma na kuendelea kuupanua kulingana na mafanikio mpaka kufikia wananchi wote.

**(c) Tamko la Sera**

(i) Mfuko utaongeza wigo ili huduma zitolewazo ziwafikie wananchi wote.

(ii) Mfuko utaboresha huduma na mafao kwa wanachama wake, ili kuweza kulipia huduma za ndani na nje, kwa ngazi zote mpaka huduma za ubingwa maalum.

### 5.10.8 Hospitali ya Taifa ya Muhimbili

**(a) Maelezo**

Hospitali ya Taifa ya Muhimbili ilianzishwa kwa Sheria ya Bunge Na. 5 ya mwaka 2000. Hii ni hospitali kuu ya rufaa na mafunzo nchini Tanzania, inayotambulika kitaifa na kimataifa, inatoa huduma za kitaalamu za tiba, utafiti na mafunzo kwa wataalamu mbalimbali wa afya. Huduma zinazotolewa zinatakiwa ziboreshwe na kupanuliwa ili ziweze kukidhi mahitaji ya sasa na baadae. Mahitaji haya yanaongezeka kutokana na mabadiliko ya kiteknolojia, kuongezeka kwa magonjwa na pia, kuongezeka kwa idadi ya watu na hatimaye kutoa huduma za ngazi ya ubingwa maalum.

**(b) Madhumuni**

Kutoa huduma za uchunguzi na tiba zilizo bora na endelevu kwa kutumia utaalamu wa kibingwa kwa wagonjwa wa rufaa na wanaohitaji huduma za ngazi ya ubingwa maalum kutoka sehemu zote nchini Tanzania na kuendeleza tafiti mbalimbali za afya.

**(c) Tamko la Sera**

(i) Hospitali itaendelea kutoa huduma bora za ubingwa na ubingwa maalum kwa wagonjwa wote kwa usawa.

(ii) Hospitali ya Taifa Muhimbili itaendeleza huduma za ubingwa na ubingwa maalum zinazotolewa hapa nchini kwa taratibu za rufaa na kupunguza idadi ya wagonjwa wanaohitaji kutibiwa nje ya nchi.

(iii) Hospitali ya Taifa Muhimbili itaendelea kushirikiana na Chuo Kikuu cha Sayansi za Afya cha Muhimbili (MUHAS) pamoja na vyuo vingine vya Sayansi za Afya katika kutoa mafunzo, ili kuchangia katika jitihada za nchi za kukidhi mahitaji ya wataalamu wa afya.

(iv) Hospitali ya Taifa Muhimbili itaendelea kufanya tafiti mbalimbali katika nyanja za afya kwa kushirikiana na taasisi nyingine, ili kuboresha kinga na tiba ya magonjwa mbalimbali.

## 5.11 Mabaraza na Vyama vya Kitaaluma

### 5.11.1 Mabaraza ya kitaaluma

**(a) Maelezo**

Mabaraza ya kitaaluma ni vyombo muhimu katika kuandaa, kuboresha na kusimamia viwango na maadili ya taaluma. Pamoja na kuwepo kwa vyombo hivi, bado maadili na viwango vya taaluma havizingatiwi na baadhi ya wanataaluma. Aidha, mabaraza haya ni dhaifu katika kutekeleza majukumu yaliyopewa. Hali hii inasababisha wananchi kukosa huduma bora wanazostahili au kucheleweshwa kupata huduma.

**(b) Madhumuni**

Kuwapa wananchi huduma iliyo bora na salama inayotolewa na wataalam wenye kuzingatia viwango na maadili ya kitaaluma.

**(c) Tamko la sera**

(i) Mabaraza ya kitaaluma yatawezeshwa kutekeleza majukumu yake kulingana na sheria, kanuni na taratibu.

(ii) Serikali itahakikisha kuwa muundo wa mabaraza unazingatia usawa wa kijinsia.

(iii) Serikali kwa kushirikiana na mabaraza ya taaluma itahakikisha kwamba wataalam wa sekta ya afya wanafanya kazi kwa kuzingatia viwango na maadili ya taaluma zao.

(iv) Mabaraza ya taaluma yataendelea kuundwa ili kuratibu wanataaluma wa sekta ya afya kulingana na mahitaji yatakayokuwepo.

### 5.11.2 Vyama vya kitaaluma

**(a) Maelezo**

Taaluma nyingi zimeanzisha vyama vyao kwa madhumuni ya kuboresha huduma zitolewazo na wanachama wake, kuboresha taaluma zao, kulinda na kutetea maslahi yao. Hata hivyo, mchango wa vyama hivyo katika kuboresha taaluma ni mdogo kutokana na udhaifu wa vyama hivyo na kutoshirikishwa

kikamilifu katika kuendeleza taaluma na kuboresha huduma katika sekta ya afya.

**(b) Madhumuni**

Kuwa na vyama imara vya kitaaluma vyenye kusimamia taaluma zao kwa maslahi ya wananchi.

**(c) Tamko la sera**

(i) Vyama vya kitaaluma vitashirikishwa katika kuendeleza taaluma na kutoa huduma bora kwa wananchi.

(ii) Serikali itashirikiana na vyama vya kitaaluma ili viweze kutekeleza wajibu wa kutoa huduma bora kwa wananchi na kulinda haki za wanachama wao.

## 6.0 MASUALA MTAMBUKA YA SERA

Masuala mtambuka ya sera ni yale ambayo utekelezaji wake unagusa sekta mbalimbali na jamii. Masuala haya yatatekelezwa kwa kushirikiana na sekta na mamlaka nyingine kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu zilizopo. Masuala mtambuka vilevile, yana maelezo, madhumuni na matamko, na ni haya yafuatayo;

### 6.1 Majanga na maafa

**(a) Maelezo**

Majanga asilia na yanayotokana na shughuli za binadamu yanasababisha maafa na upotevu wa maisha ya watu, mali na uharibifu wa mazingira. Pamoja na kutokea majanga na maafa mara kwa mara, huduma za usafirishaji wagonjwa pamoja na huduma za dharura za kukabiliana na athari za kiafya za maafa hayo bado ni dhaifu.

**(b) Madhumuni**

Kuchangia na kuimarisha kisekta hatua za kupunguza athari za majanga na maafa kulingana na Sera ya Taifa ya Menejimenti ya Maafa.

**(c) Tamko la sera**

(i) Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali itaimarisha na kuandaa taratibu na mifumo ya kuzuia, kujiandaa na kukabiliana na majanga na maafa, hususan yale yatokanayo na huduma zitolewazo katika sekta ya afya.

(ii) Serikali itaimarisha na kuweka utaratibu wa kuratibu, kutekeleza na kutathmini shughuli endelevu za kudhibiti matukio ya majanga na maafa, hususan yale yatokanayo na huduma zitolewazo katika sekta ya afya.

(iii) Serikali kwa kushirikiana na wadau itaboresha na kuimarisha uwezo wa wataalam wa sekta ya afya na ustawi wa jamii katika kukabiliana na majanga na maafa, ikiwemo upatikanaji wa vyombo vya usafiri.

## 6.2 Ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa

**(a) Maelezo**

Ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa unalenga katika kushirikisha nchi na nchi juu ya utoaji huduma bora zinazokubalika kwa mataifa husika. Tanzania imeendelea kuimarisha ushirikiano huo, ili kukabiliana na changamoto kama za; mabadiliko ya kiteknolojia ulimwenguni, matatizo ya magonjwa mapya yanayoibuka na yale yanayojirudia, kuzuka kwa magonjwa ya milipuko ikiwa ni pamoja na kujitokeza kwa usugu wa vimelea vya magonjwa katika mataifa mbalimbali. Ushirikiano huu wa Tanzania na mataifa mengine umeendelea kuimarishwa tangu kupata uhuru.

Hata hivyo, mabadiliko yanayosababishwa na utandawazi pamoja na teknolojia mpya za kukabili magonjwa, unafanya kuwepo kwa ulazima wa kuboresha ushirikiano wa kikanda na kimataifa, kulingana na viwango vya utoaji huduma vinavyokubalika.

**(b) Madhumuni**

Kujenga, kuendeleza na kuimarisha ushirikiano wa kikanda, kimataifa na mashirika ya kimataifa katika kuboresha huduma za afya.

**(c) Tamko la sera**

(i) Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali itajenga, itaendeleza, kuimarisha na kudumisha ushirikiano wa kikanda, kimataifa na mashirika ya kimataifa.

(ii) Serikali itaendelea kupitia na kuridhia mikataba ya kikanda na kimataifa, ili kuboresha huduma za afya.

(iii) Serikali itaweka miongozo na kusimamia kikamilifu raslimali zinazotolewa kupitia ushirikiano wa kikanda na kimataifa.

## 6.3 UKIMWI

**(a) Maelezo**

Serikali inafanya juhudi kubwa kukabiliana na janga la UKIMWI. Hata hivyo, kutokuwepo mwitikio sahihi wa kukabiliana na janga la UKIMWI miongoni mwa wananchi, kunaendelea kuathiri juhudi za kukabiliana na janga hili. Hali hii, inaendelea kuathiri nguvu kazi, kuongeza vifo, yatima, umaskini na gharama za matibabu pamoja na kuathiri ustawi, uchumi na usalama wa taifa.

**(b) Madhumuni**

Kudhibiti maambukizi na ya Virusi vya UKIMWI nchini na kutoa matunzo na tiba ya kupunguza makali ya UKIMWI.

**(c) Tamko la Sera**

(i) Serikali itaendelea kushirikiana na wadau katika kukabiliana na janga la UKIMWI katika nyanja zote zikiwemo, kinga, huduma za tiba katika vituo vya kutolea huduma za afya na majumbani, ili kupunguza athari zinazosababishwa na VVU/UKIMWI.

(ii) Serikali itaweka mikakati endelevu inayozingatia kikamilifu mazingira halisi ya kukabiliana na UKIMWI katika jamii na sehemu za kazi.

(iii) Serikali itaweka utaratibu wa kisheria unaolinda jamii dhidi ya maambukizi ya VVU/UKIMWI na kulinda haki za waathirika, waathiriwa na watoa huduma.

(iv) Serikali itasimamia na kuratibu tafiti mbalimbali zenye kuchangia katika kudhibiti janga la UKIMWI.

(v) Serikali itahakikisha kuwa shughuli za mapambano dhidi ya UKIMWI zinaunganishwa katika utoaji wa huduma za afya za kila siku.

(vi) Serikali itaendelea kuimarisha uratibu wa shughuli za UKIMWI zinazotolewa na wadau mbalimbali.

(vii) Serikali itaimarisha utoaji wa huduma kwa wagonjwa wa UKIMWI ambao unazingatia utunzaji wa siri na kuondoa unyanyapaa.

## 6.4 Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEKNOHAMA)

**(a) Maelezo**

Serikali inatambua kuwa, teknolojia ya habari na mawasiliano ni nyenzo muhimu katika kusukuma maendeleo ya taifa, hasa katika kuimarisha mfumo wa utoaji huduma katika sekta ya afya. Maendeleo katika TEKNOHAMA yanagusa kila sekta na Serikali inalazimika kuhakikisha kwamba sekta ya afya iko sanjari katika matumizi sahihi ya teknolojia hii, ili kuongeza tija na ufanisi.

Hata hivyo, ni watalaam wachache sana wa sekta ya afya wenye ujuzi wa TEKNOHAMA. Aidha, ufinyu wa bajeti umefanya Serikali ishindwe kutoa mafunzo ya TEKNOHAMA sambamba na kasi ya mahitaji.

**(b) Madhumuni**

Kutumia TEKNOHAMA katika kuongeza tija, ufanisi na ubora wa huduma za afya nchini.

**(c) Tamko la sera**

(i) Serikali itaweka na kutumia mfumo endelevu wa habari na mawasiliano katika shughuli za sekta ya afya.

(ii) Serikali itaandaa kanuni, miongozo na taratibu za kuendesha na kusimamia TEKNOHAMA katika sekta ya afya.

(iii) Serikali itaandaa mafunzo endelevu ya TEKNOHAMA kwa watumishi wote wa sekta ya afya.

## 6.5 Utawala bora

**(a) Maelezo**

Utawala bora ni mfumo wa utendaji unaozingatia uwazi, uadilifu na uwajibikaji, ili kuleta ufanisi katika sehemu za kazi. Juhudi zimefanyika katika kuimarisha ufanisi na uwajibikaji katika sehemu za kazi. Hata hivyo, bado kuna kutowajibika vya kutosha miongoni mwa viongozi na watumishi. Aidha, nidhamu na maadili ya baadhi ya viongozi na watumishi imeshuka na kumekuwepo na vitendo vya rushwa na lugha isiyoridhisha kwa wateja. Vitendo hivyo, vinawanyima wananchi haki zao za msingi. Hali hii, imesababisha malalamiko mengi kwa sekta ya afya.

**(b) Madhumuni**

Kujenga na kuimarisha misingi ya utawala bora katika utoaji huduma za afya katika ngazi zote, ili kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora kama inavyostahili.

**(c) Tamko la sera**

(i) Serikali itaandaa na kutekeleza mkakati wa kuziba mianya ya rushwa katika sehemu za kutolea huduma za afya.

(ii) Serikali itasimamia sheria, kanuni na taratibu zitakazowezesha kuimarika kwa uwajibikaji, uwazi na maadili katika utoaji huduma za afya.

(iii) Serikali itaimarisha mawasiliano na wadau, vyombo mbalimbali,

mabaraza, na vyama vya kitaaluma, bodi na kamati za afya ili kujenga uhusiano mzuri na uwazi katika utendaji kazi.

(iv) Watumishi wa Sekta ya Afya watahamasishwa na kuelimishwa juu ya namna ya kukabiliana na rushwa mahali pa kazi kwa kuzingatia maadili mema ya taaluma zao.

(v) Serikali kwa kushirikiana na mabaraza pamoja na vyama vya taaluma itaweka miongozo, taratibu na mikataba ya utumishi inayozingatia uadilifu na maadili mema ya utumishi.

## 6.6 Jinsia

### (a) Maelezo

Serikali imefanya jitihada kubwa katika kuzingatia jinsia na makundi maalum katika utoaji huduma za afya nchini. Hata hivyo, juhudi zaidi zinahitajika kwani mahitaji ya makundi maaalum kwa mfano; watoto, wanawake, wazee, watu wenye ulemavu na wasiojiweza yanaongezeka. Hii inatokana na maendeleo katika mawasiliano na teknolojia katika utoaji huduma za afya kwa makundi hayo. Aidha, huduma za afya zinazotolewa hazikidhi mahitaji kama inavyostahili.

### (b) Madhumuni

Kutoa huduma za afya kwa usawa na uwiano kwa kuzingatia jinsia na mahitaji maalum ya makundi mbalimbali katika jamii.

### (c) Tamko la sera

(i) Serikali itaandaa sheria, kanuni, miongozo na taratibu za utoaji wa huduma za afya kwa kuzingatia jinsia na mahitaji ya makundi maalum.

(ii) Serikali kwa kushirikiana na wadau itashirikisha makundi maalum kwa kuzingatia jinsia katika maandalizi ya mipango na utekelezaji wake.

(iii) Serikali kwa kushirikiana na wadau itatoa huduma za afya kwa kuzingatia jinsia na mahitaji ya makundi maalum.

(iv) Serikali itaweka mazingira mazuri yatakayoongeza usawa wa kijinsia katika kufanya maamuzi ndani ya vyombo mbalimbali vya sekta ya afya kama vile; Bodi na Kamati za afya.

### 6.7 Kupunguza Umaskini

**(a) Maelezo**

Dira ya Taifa ya mwaka 2025, inalenga kukuza uchumi na kupunguza umaskini kupitia MKUKUTA ambao ni Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania. Utekelezaji wa mkakati huu pamoja na kupunguza umaskini na kuongeza kipato vilevile, unazingatia suala zima la kuongeza ubora wa maisha na utawala bora. Mkakati huu umeandaliwa kwa kuwashirikisha wananchi na wadau wengine.

**(b) Madhumuni**

Kuhakikisha wananchi wanahamasika kuchukua jukumu la kuboresha afya zao, kwa kutumia malengo ya MKUKUTA, ambayo yataongeza kipato na kupunguza umaskini.

**(c) Tamko la sera**

(i) Kazi zote za huduma ya afya zitazingatia malengo yaliyoainishwa kwenye MKUKUTA.

### 6.8 Haki za Binadamu

**(a) Maelezo**

Haki za binadamu ni muhimu zizingatiwe katika utoaji wa huduma yeyote. Kila mtu anayo haki ya kupata huduma za afya bila kujali jinsia, kabila na nafasi yake katika jamii.

**(b) Madhumuni**

Kutoa huduma za afya katika misingi ya haki ya binadamu bila ubaguzi.

**(c) Tamko la sera**

(i) Serikali itahakikisha kuwa watoa huduma za afya wanazingatia haki za binadamu wakati wa kuwahudumia wananchi.

(ii) Serikali kwa kushirikiana na wadau wengine itatoa miongozo ya kuondoa unyanyapaa katika kutoa huduma za afya.

### 6.9 Rushwa

#### (a) Maelezo

Rushwa ni mojawapo ya vikwazo ambavyo vimekuwa vinawafanya baadhi ya wananchi kukosa huduma za afya ambazo ni haki yao. Juhudi zimekuwa zikifanyika kuwaelimisha watoa na wapokea huduma za afya jinsi ya kuepuka tatizo hili. Hata hivyo, rushwa imeendelea kuwa mojawapo ya kero katika utoaji wa huduma za afya nchini.

#### (a) Madhumuni

Kutokomeza vitendo vya rushwa katika utoaji wa huduma za afya katika ngazi zote.

#### (b) Tamko la sera

(i) Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali itaendelea kutoa elimu kwa watoa huduma za afya na wananchi kwa ujumla kuachana na vitendo vya kutoa na kupokea rushwa.

### 6.10 Mazingira

#### (a) Maelezo

Neno mazingira ni neno pana sana, linajumuisha hewa, ardhi, maji, mimea, maisha ya wanadamu na wanyama ikiwa ni pamoja na mienendo na tabia za jamii na jinsi wanavyohusiana, Pia, majengo, mashine na vifaa vingine vinavyotengenezwa na binadamu viwe vigumu, vya maji maji, gesi, joto, sauti, mawimbi, mionzi na vinginevyo vinahusika katika jumuisho la neno mazingira.

Maisha ya binadamu na viumbe vyote vilivyo hai pamoja na mimea hutegemea uhifadhi mzuri wa mazingira.

Serikali kwa kutambua umuhimu wa kuhifadhi mazingira imekuwa ikielimisha jamii kutunza na kulinda mazingira katika maeneo yote wanakoishi kwa kutumia kampeni mbalimbali kama vile; kupanda miti, usikate miti hovyo, kulinda vyanzo vya maji, kulinda misitu ya asili, kutokulima na kuchunga wanyama kwenye maeneo yanayoweza kusababisha mimomonyoko, kuzuia uchafuzi wa hewa na kutotupa takataka ngumu (plastiki) hovyo.

Pamoja na juhudi nzuri za serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, bado

wananchi wengi hawajalipa uzito wa kutosha suala la kuhifadhi na kulinda mazingira kwa faida yao na vizazi vijavyo.

Juhudi za makusudi zinahitajika ili kuweza kubadilisha mtizamo na tabia za wananchi, ili waweze kuthamini, kulinda na kutunza mazingira.

**(b) Madhumuni**

Kuwa na utaratibu mzuri na endelevu wa kuhifadhi kutunza na kulinda mazingira kwa faida ya afya ya wananchi na vizazi vijavyo.

**(c) Tamko la Sera**

(i) Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali itaendelea kuelimisha watoa huduma za afya, umuhimu wa kutunza na kulinda mazingira katika maeneo yao.

(ii) Serikali itapitia na kutunga sheria, miongozo, kanuni na taratibu zitakazowezesha kuhifadhi, kutunza na kulinda mazingira.

(iii) Serikali itaendelea kuwashirikisha wananchi katika kusimamia na kulinda mali za asili zilizoko katika maeneo yao.

## 7.0 MUUNDO WA KITAASISI

Sekta ya Afya ina lengo la kutoa huduma muhimu za afya zilizo bora na endelevu zenye uwiano na unafuu pamoja na kuzingatia jinsia. Mfumo wa huduma za afya utazingatia upatikanaji wa aina nne (4) zote za huduma za afya katika kila ngazi. Huduma hizo ni zile za; uboreshaji afya kinga, tiba na utengemao.

Ili kufikia lengo hili, kunahitajika wataalam wa kutosheleza mahitaji ya huduma hizi. Aidha ushirikishwaji wa wananchi, sekta binafsi, asasi zisizo za Serikali na sekta nyingine utahitajika kuimarishwa, kwani sekta ya afya pekee haiwezi kukidhi mahitaji yote ya huduma za afya kwa wananchi. Dhana ya kupeleka madaraka kwa wananchi itazingatiwa.

Ushiriki wa sekta nyingine katika kutoa huduma za afya kwa kuzingatia maelekezo ya sera hii, kunahitaji kuongozwa na muundo wa kitaasisi unaojulikana kwa kila sekta shiriki. Muundo huu utaepusha urasimu na mwingiliano wa majukumu wakati wa utekelezaji wa sera hii. Muundo na majukumu yanaanzia ngazi ya kaya hadi taifa.

### 7.1 Muundo na majukumu ya utoaji huduma katika kila ngazi:

#### 7.1.1 Kaya, Mtaa/Kijiji:

(i) Ni wajibu wa kila mwananchi kutunza na kuhifadhi afya yake na ya familia. Vilevile, kutokufanya au kutokutenda jambo litakaloathiri afya za wengine au majirani zao.

(ii) Ni wajibu wa wananchi kuchangia kwa hali na mali huduma za afya, kulinda na kutunza mali katika vituo vyao vya kutolea huduma za afya.

(iii) Kamati ya huduma za jamii ya kijiji/mtaa ina wajibu wa kushirikisha wananchi wote katika kutoa mawazo na maamuzi kuhusu uboreshaji na uendeshaji wa huduma za afya.

(iv) Kila kijiji kitakuwa na zahanati. Kijiji chenye kituo cha afya, hakitakuwa na haja ya kuwa na zahanati. Huduma zitakazotolewa katika zahanati ni pamoja na; uboreshaji wa afya (health *promotion*), kinga, tiba na utengemao (*rehabilitation*).

(v) Jengo la zahanati litakuwa na vyumba na nafasi ya kutosheleza mahitaji ya huduma muhimu zinazotakiwa kutolewa katika kituo hicho. Zahanati

itakuwa imekamilika kutoa huduma kwa kuwa na huduma ya maji, nishati, vyoo na nyumba za wafanyakazi. Michoro maalum ya zahanati itatolewa na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii.

(vi) Kwa kushirikisha watumiaji wa huduma, kila zahanati itakuwa na wataalam wa kutosheleza mahitaji ya huduma zitolewazo katika ngazi hiyo.

(vii) Kila zahanati itakuwa na Mpango Shirikishi wa utoaji huduma za afya wa kila mwaka. Kamati ya Zahanati pamoja na wananchi watawajibika kutekeleza mpango huo.

### 7.1.2 Kata

Serikali kwa kupitia Ofisi ya Mtendaji wa Kata itakuwa na wajibu wa kushirikisha wananchi kupitia Kamati za Kituo cha Afya, wa kuboresha huduma za afya. Kwa kuwa kituo cha afya ni ngazi ya kwanza ya rufaa ya wagonjwa kutoka zahanati zilizopo katika kata, kituo hicho ni budi kiwe na wataalam wa kutosheleza mahitaji ya huduma zote katika ngazi hiyo.

Jengo la Kituo cha Afya litakuwa na vyumba na nafasi ya kutosheleza mahitaji ya huduma muhimu zinazotakiwa kutolewa katika kituo hicho. Kituo cha Afya kitakuwa kimekamilika kutoa huduma kwa kuwa na huduma ya maji, nishati, vyoo na nyumba za wafanyakazi. Michoro maalum ya Kituo cha Afya itatolewa na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii.

Kila kituo cha afya kinahitaji kuwa na chombo cha usafiri na mawasiliano na hospitali ya wilaya ili kukidhi mahitaji ya rufaa ya wagonjwa kutoka kwenye zahanati kwenda hospitali ya wilaya.

Kila kituo cha afya kitakuwa na Mpango Shirikishi wa Afya kuelekeza utoaji huduma za afya wa kila mwaka. Kamati ya Afya ya Kituo na wananchi watawajibika kutekeleza mpango huo.

### 7.1.3 Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa na za Jiji

Halmashauri ni kitovu cha kutolea huduma za afya na kusimamia ubora wa huduma hizo. Ina mamlaka ya kupokea taarifa, kupanga, kuratibu, kutekeleza, kufuatilia na kutathmini huduma za afya, ikishirikiana na jamii pamoja na wadau katika ngazi zote. Ngazi hii itasimamia moja kwa moja vituo vyote vya kutolea huduma za afya, vilivyomo katika halmashauri hiyo.

Kila halmashauri itakuwa na mpango shirikishi wa afya wa kila mwaka. Mpango utakuwa mjumuisho wa mipango ya zahanati, vituo vya afya, hospitali ya wilaya na Timu ya Uongozi wa Huduma za Afya ya Halmashauri. Hospitali itatoa huduma zote pamoja na za ubingwa kwenye maeneo ya watoto, kina mama, magonjwa ya kawaida na upasuaji.

Aidha, ni wajibu wa halmashauri kuanzisha Bodi ya Huduma za Afya na Kamati za vituo vya kutolea huduma za afya, ili kushirikisha wananchi katika kusimamia na kumiliki raslimali za afya. Bodi na Kamati hizo zinawajibika kwa Halmashauri kupitia Kamati ya Huduma za Jamii.

Pamoja na kuwa na vituo vya afya, zahanati na hospitali, mfumo wa huduma za kutembelea maeneo yaliyo nje ya vituo zitaimarishwa ili kuwasaidia wale ambao hawawezi kuja vituoni kupata huduma.

### 7.1.4 Mkoa

Jukumu la mkoa ni kutoa huduma za rufaa kwa mkoa na pia kufuatilia utekelezaji wa sera, sheria, kanuni na miongozo mbalimbali, ikiwa ni pamoja na; ushauri wa kitaalamu, kusimamia, kuratibu na kudhibiti viwango na ubora wa huduma za afya zitolewazo ngazi ya Halmashauri. Ngazi hii itasimamia moja kwa moja hospitali zote zilizopo katika mkoa huo. Aidha, Serikali itaunda Bodi za kusimamia hospitali za mikoa. Kiongozi atakuwa na ngazi ya Mkurugenzi.

Katika kutekeleza majukumu yake, ngazi ya mkoa itahitaji kuwa na Timu ya Uongozi wa Huduma za Afya ya Mkoa yenye nyenzo muhimu na wataalam katika maeneo yafuatayo:

(i) Huduma muhimu za afya kulingana na Kitita cha Huduma Muhimu za afya.

(ii) Uandaaji wa mipango shirikishi ya afya ya vituo vyote vya kutolea huduma za afya katika mkoa.

(iii) Matumizi bora ya raslimali zote za huduma za afya (fedha, watu, dawa, vifaa, majengo, muda na nafasi).

(iv) Ukusanyaji, uchambuzi, tafsiri na matumizi ya takwimu za afya pamoja na kuandaa taarifa za kupeleka ngazi za juu na mrejesho kwa ngazi zote za ukusanyaji wa takwimu.

(v) Utafiti unaolenga kutumia matokeo kwa ajili ya kuboresha huduma

muhimu za afya.

(vi) Maendeleo ya watumishi wa sekta ya afya pamoja na kuendeleza utaalam wa fani mbali mbali za huduma za afya katika mkoa.

(vii) Afya ya mazingira.

Hospitali ya Mkoa itaendeshwa na Timu ya Uendeshaji ya Hospitali ikiongozwa na Daktari Mfawidhi wa Hospitali ambaye ataitwa Mkurugenzi Msaidizi wa Huduma za Tiba Mkoani. Jukumu kuu la Timu hii ni, kupanga na kutoa huduma bora za afya zinazokidhi mahitaji ya wagonjwa katika hospitali hiyo. Timu hii itawajibika kwa Mganga Mkuu wa Mkoa ambaye ataitwa Mkurugenzi wa Huduma za Afya wa Mkoa. Aidha, Mkurugenzi huyo ataongoza Timu ya Afya ya Mkoa ambayo itawajibika kwa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii katika masuala ya kitaalam. Hospitali itakuwa na madaktari bingwa wa aina zote.

### 7.1.5 Kanda

Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii itakuwa na vituo vya kanda katika kuwezesha uboreshaji wa huduma za afya endelevu, kutokana na kuendesha mafunzo mbali mbali, ushauri, usimamizi na ufuatiliaji na utafiti. Mifano ya vituo vingine vya Wizara katika kanda ni; Bohari za Dawa, Hospitali za Rufaa na Maalum, vituo vya Damu Salama, vituo vya Mkemia Mkuu wa Serikali na Mamlaka ya Chakula na Dawa. .

Utumiaji wa vituo hivi vya kanda ni sehemu muhimu ya kiutendaji katika kutoa na kuboresha huduma, na ni kiungo muhimu kati ya Wizara Makao makuu na halmashauri kupitia mikoa. Serikali itaweka na kuimarisha mfumo wa vituo vya kanda kama kiungo muhimu cha kuratibu, kutolea, kusambaza na kuboresha huduma muhimu za afya katika mikoa na halmashauri zilizoko ndani ya kanda husika.

### 7.1.6 Taifa

Jukumu la Wizara ni kuandaa, kusimamia, kutafsiri na kuratibu utekelezaji wa sera, sheria, kanuni, miongozo na viwango vya huduma za afya katika ngazi zote za kutolea huduma.

Wizara Makao Makuu itakuwa na idara mbali mbali zenye majukumu maalum ya kuratibu na kufuatilia hali ya afya ya watanzania na huduma za afya nchini. Majukumu haya yatawezeshwa kutokana na jukumu lingine muhimu la Wizara la uchambuzi na tafsiri ya sera na tafiti mbali mbali zinazofanywa kwa lengo la

kuboresha huduma za afya nchini.

Ili kuwezesha jukumu hili, Wizara itakuwa na kitengo maalum chenye jukumu la kufanya kazi muhimu ya uchambuzi makini na tafsiri ya sera, tafiti mbalimbali zinazofanywa nchini na taarifa zingine muhimu zinazohusu hali ya afya na huduma zinazotolewa. Kitengo kitakuwa na wataalam wenye uwezo na uzoefu wa kuwezesha mijadala ya sera, matokeo ya tafiti, taarifa mbalimbali za usimamizi na ufuatiliaji wa huduma za afya nchini na kuishauri Wizara ili kutoa maamuzi ya kisera.

Kitengo hiki kitashirikiana na vituo vya kanda ili kuwezesha utekelezaji, kwa vitendo, uboreshaji wa huduma za afya nchini. Vituo vya kanda vitawezesha uendelezaji wa uwezo wa wataalam katika ngazi za chini, kuboresha huduma bora za afya kwa uendelevu.

Aidha, Serikali kwa kupitia bodi zake inasimamia huduma za afya zinazotolewa katika hospitali za Wilaya, Hospitali za Rufaa za Mikoa na Maalum ngazi ya Taifa. Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa itaendelea kutoa huduma za afya kwa kuzingatia Sera ya kupeleka madaraka na raslimali karibu na wananchi.

## 7.2 Ushirikiano na wadau mbalimbali

Katika kutekeleza sera hii, Serikali itashirikiana na wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja na; mashirika ya dini, sekta binafsi, asasi zisizo za kiserikali, mashirika ya kimataifa na nchi wahisani.

### 7.2.1 Mashirika ya dini

Serikali itashirikiana na mashirika ya dini yatoayo huduma bila faida katika kutoa huduma za afya kuanzia ngazi ya zahanati hadi taifa. Aidha, Serikali itatathmini vituo vya kutolea huduma za afya. Ili kuhakiki ubora wa huduma zitolewazo.

### 7.2.2 Sekta binafsi

Serikali itashirikiana na sekta binafsi katika kutoa huduma za afya kuanzia ngazi ya zahanati hadi rufaa. Aidha, Serikali itatathmini vituo vya kutolea huduma za afya. ili kuhakiki ubora wa huduma zitolewazo.

### 7.2.3 Asasi zisizo za kiserikali

Serikali itaendelea kushirikiana na asasi hizi. Katika ushirikiano huu, asasi zote zinazotoa huduma za afya moja kwa moja na zile zinazojadiliana na Serikali, wakati wa kuweka mikakati na miongozo mbalimbali, hazina budi kuzingatia taratibu zote pamoja na sheria na matamshi ya sera hii.

### 7.2.4 Mashirika ya kimataifa na nchi wahisani

(i) Mashirika ya kimataifa na nchi wahisani zitaendelea kushirikishwa katika juhudi za Serikali na wananchi za kuboresha huduma za afya kwa kutoa msaada wa fedha na teknolojia.

(ii) Serikali itaomba msaada wa kitaalam pale unapohitajika kwa lengo la kujenga uwezo wa wataalam wetu.

## 8.0 MFUMO WA KISHERIA

Mfumo wa huduma za afya unajumuisha huduma zitolewazo na Serikali kuu kupitia Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na kukasimiwa kwa Serikali za mitaa, mashirika ya dini na ya kujitolea, vyama na watu binafsi. Aidha, huduma za tiba asilia na tiba mbadala zinatambulika ndani ya sera hii. Katika kutoa huduma hizi, mfumo utakaotambulika kisheria utakuwa kwenye ngazi zifuatazo: taifa, kanda, mkoa, wilaya, kata, kijiji na kaya. Muundo huu wa kisheria utazingatia miundo inayokidhi utekelezaji wa maeneo muhimu ya huduma za afya ambayo ni uboreshaji afya, kinga ya magonjwa, tiba ya magonjwa na huduma za utengemao katika ngazi zote.

Kwa sasa hakuna muundo wa kisheria mmoja ambao unasimamia huduma za afya nchini. Kumekuwa na vyombo mbalimbali ambavyo vinatambuliwa kiutawala tu, kwa mfano; hospitali za wilaya, mkoa, rufaa, Timu za Uendeshaji wa Huduma za Afya za Mkoa na Halmashauri, hivyo, kuna umuhimu wa kuwa na sheria ambayo itatambua vyombo hivyo kisheria. Uendeshaji na usimamizi wa huduma za afya hapa nchini utafuata taratibu za sheria zilizopo na zitakazotungwa.

### 8.1 Sheria za kusimamia huduma za afya

Sheria zilizopo zitaendelea kutumika ikiwa zinakidhi maelekezo na matamko ya sera hii. Sheria zisizokidhi mahitaji ya sera hii zitapitiwa na kufanyiwa marekebisho au kufutwa. Aidha, sheria mpya zitatungwa ili zikidhi maelekezo na matamko mapya ya Sera ambayo hayakutajwa katika sheria zilizopo.

### 8.2 Vyombo vya kisheria vya kusimamia huduma za afya

Kutakuwepo na vyombo vya kisheria katika ngazi zote ili kusimamia huduma za afya katika maeneo hayo kwa mujibu wa sheria. Vyombo hivyo ni; mabaraza na bodi za kitaaluma za kusimamia taaluma na maadili katika utoaji wa huduma za afya ngazi zote. Aidha, kutakuwepo bodi na au kamati za afya ngazi zote ili kusimamia huduma za afya kwenye maeneo hayo kwa mujibu wa sheria. Bodi au kamati hizo zitateuliwa na mamlaka husika au aliyekasimiwa madaraka hayo na Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii.

Bodi zitasimamia huduma za afya ngazi ya halmashauri na hospitali za mkoa, rufaa na maalum. Vilevile, kutakuwepo na kamati katika ngazi ya hospitali ya wilaya itakayosimamia huduma zinazotolewa katika hospitali hiyo.

Kamati za ngazi ya kata, kijiji/mtaa na jamii zitasimamia huduma ngazi ya zahanati na vituo vya afya. Kamati hizi ndizo zitakazoainisha na kutambua maskini wasiojiweza na watakaohitaji kupatiwa huduma bila malipo.

Kutakuwepo timu za kitaalam za kusimamia taaluma na maadili katika utoaji wa huduma za afya ngazi zote. Miongozo ya timu, majukumu na hadidu za rejea zitatolewa na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii.

Serikali inatambua kuwepo kwa sekta binafsi zikijumuisha Mashirika ya dini na ya kujitolea. Sekta hii itaendelea kutoa huduma za afya ikishirikiana na Serikali kwa mujibu wa sheria na kanuni zinazosimamia na kuelekeza ushirikiano huo. Aidha, Serikali itaendelea kuwasiliana na uongozi wa sekta binafsi ili kuimarisha ushirikiano na maelewano katika utoaji wa huduma za afya kwa ufanisi.

## 8.3 Sheria ya kusimamia vyuo vya mafunzo ya afya

Vyuo vya mafunzo ya afya vya Serikali vitatambuliwa kisheria na kuundiwa bodi za usimamizi chini ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii

# 9.0 MWISHO

Sera hii ni ya kuboresha huduma za afya ya jamii. Afya bora ni mtaji wa kukabiliana na umaskini, kuleta maisha bora kwa wote na kupunguza kasi ya kuenea kwa UKIMWI na magonjwa mengine yakiwemo ya kuambukiza, yasiyo ya kuambukiza na milipuko.

Sera imeelekeza namna ya kutekeleza na kupima ufanisi wa sekta hii na pia, ufanisi wa kitaifa hasa kutumia vigezo vya afya ya mama na mtoto. Kasoro zitakazojitokeza zitaainishwa kwa njia mbalimbali ikiwa ni pamoja na utafiti, ili kupatiwa ufumbuzi. Ili sera hii itekelezwe kwa ufanisi ni tegemeo kuwa kutakuwepo upatikanaji wa fedha za kutosha kwa huduma muhimu, kuwepo wataalam wenye uwezo na ari ngazi zote, upatikanaji wa vifaa na teknolojia ya kisasa, pamoja na kudhibiti kasi ya milipuko na maafa mbalimbali. Kila mwananchi na kila mdau anategemewa kutoa mchango wake katika kufikia lengo la sera hii.